JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI
WA UMMA NA UTAWALA BORA





# HOTUBA

**YA WAZIRI WA NCHI – OFISI
YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI
WA UMMA NA UTAWALA BORA,
MHESHIMIWA RIDHIWANI J. KIKWETE
(MB) KUHUSU MAKADIRIO YA
MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA
KWA MWAKA 2026/27**

Aprili 2026

**Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

Mji wa Serikali Mtumba Mtaa wa Utumishi
S.L.P. 670, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 (0) 26 216 0240
Barua pepe: ps@utumishi.go.tz

**www.utumishi.go.tz**

OR_Utumishi

Ofisi ya Rais-UTUMISHI

ofisi_ya_rais_utumishi

# UONGOZI WA OFISI YA RAIS, IKULU NA MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA



**MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania



**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE**
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora



**MHE.  REGINA N. QWARAY**
Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora



**BAL. DKT. MOSES M. KUSILUKA**
Katibu Mkuu Kiongozi



**BW. MULULI M. MAHENDEKA**
Katibu Mkuu, Ikulu



**BW. JUMA S. MKOMI**
Katibu Mkuu, UTUMISHI



**BW. XAVIER M. DAUDI**
Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

# YALIYOMO


| | | | |
|---|---|---|---|
| UTANGULIZI | | | 1 |
| 1. | MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/26 | | 11 |
| | 1.1. | Ofisi ya Rais - Ikulu na Taasisi Zake | 11 |
| | 1.2. | Fungu 33 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma | 43 |
| | 1.3. | Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Taasisi Zake | 47 |
| | 1.4. | Fungu 67 - Ofisi ya Rais, Sekretari ya Ajira katika Utumishi wa Umma | 61 |
| | 1.5. | Fungu 94 - Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma | 65 |
| | 1.6. | Fungu 04 - Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa | 68 |
| 2. | MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2026/27 NA MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA | | 72 |
| | 2.1. | Ofisi ya Rais - Ikulu na Taasisi Zake | 72 |
| | 2.2. | Fungu 33 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma | 84 |
| | 2.3. | Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Taasisi Zake | 86 |
| | 2.4. | Fungu 67 - Ofisi ya Rais, Sekretari ya Ajira katika Utumishi wa Umma | 95 |
| | 2.5. | Fungu 94 - Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma | 97 |
| | 2.6. | Fungu 04 - Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa | 99 |
| 3. | MAJUMUISHO | | 101 |

4. VIAMBATISHO 108

4.1. Kiambatisho 1: Takwimu za Uchunguzi kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 108

4.2. Kiambatisho 2: Orodha ya Taasisi za Umma zilizowekewa Mfumo wa Masijala Mtandao (*Keyword File Classification System*) kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026 109

4.3. Kiambatisho 3: Orodha ya Taasisi za Umma zilizowekewa Mfumo wa Utunzaji wa Kumbukumbu za Kiutendaji ((*e-File Management System*) kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026 111

4.4. Kiambatisho 4: Orodha ya Taasisi zilizowezeshwa Kutengeneza Mwongozo wa Kuhifadhi na Kutengeneza Kumbukumbu kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026 112

4.5. Kiambatisho 5: Orodha ya Taasisi za Umma zilizofanyiwa Mafunzo ya Utunzaji wa Kumbukumbu kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026 113

# UTANGULIZI

**1. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka 2025/26 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2026/27 ya Ofisi ya Rais: Ikulu (Fungu 20 na 30); Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33); Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (Fungu 32); Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67); Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94); na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa (Fungu 04).

**2. Mheshimiwa Spika,** kama ilivyo ada naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na neema kwa kutuwezesha kuwa na afya njema na kuendelea kuijalia nchi yetu amani, utulivu na mshikamano ambazo ni tunu zinazotuwezesha kushiriki katika mkutano huu wa tatu (3) wa Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**3. Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini kusimamia Utumishi wa Umma kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora, Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali na hatimaye kuwa na Utumishi wa Umma unaowajibika, jumuishi na wenye matokeo.




1. Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa awamu ya pili, Ikulu Chamwino, Dodoma, tarehe 3 Novemba 2025.

Aidha, niwashukuru Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais; Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; kwa kazi kubwa wanayofanya ya kumsaidia Rais na Amiri Jeshi Mkuu kutekeleza majukumu yake ya kusukuma maendeleo ya Taifa letu na kuiweka nchi katika hali ya usalama na amani kwa lengo la kuweka tabasamu kati mioyo ya Watanzania. Vilevile, ninawashukuru viongozi wangu wote kwa maelekezo, ushauri na miongozo wanayonipatia ambayo imenisaidia kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi mkubwa.

**4. Mheshimiwa Spika,** naomba kutumia fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mwelekeo wa nchi kwa kuanzisha hatua za kufikia malengo ya DIRA 2050 aliyoizindua Julai 2025 pamoja na kuanza utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 aliyoitumia wakati wa kuomba kura kwa Watanzania kwa kuwaahidi pamoja na mambo mengine kuweka Utawala Bora na Utumishi wa Umma ulioboreshwa na unaowalenga wananchi katika utoaji huduma kwa umma. Maboresho makubwa yaliyoelekezwa katika Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ikiwemo haya ya mifumo ya kiutawala na usimamizi wa rasilimaliwatu ya kidijitali, ni wazi yanaonyesha nia ya dhati ya Mhe. Rais katika ujenzi wa Tanzania njema.

**5. Mheshimiwa Spika,** Maboresho hayo yataleta mageuzi ya kiutendaji na utoaji wa huduma katika utumishi wa umma, na huo ni uhakikisho kuwa nchi ipo katika njia sahihi ya kufikia malengo tuliyojiwekea katika mipango yetu ya kitaifa chini ya uongozi thabiti wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Asante sana, Jemedari wetu.





1. Mhe. Bal. Dkt. Emmanuel John Nchimbi, akiapishwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ikulu Chamwino, Dodoma, tarehe 3 Novemba 2025.
2. Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.) akiapishwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ikulu Chamwino, Dodoma, tarehe 14 Novemba 2025.







1 - 2: Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akizindua Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Julai 2025, Dodoma.

**6. Mheshimiwa Spika,** kipekee nampongeza Mheshimiwa Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kwake katika nafasi hiyo muhimu katika nchi na kwa uchapakazi wake mahiri na uzalendo wenye lengo la kuliletea Taifa letu maendeleo. Tunamuahidi utii kwenye maelekezo yake na weledi katika utekelezaji ili kuchangia ipasavyo katika maendeleo na ustawi wa Taifa letu. Halikadhalika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuchaguliwa tena kuiongoza Zanzibar. Hakuna shaka kwamba ushupavu, ubunifu wake na jitihada zake za kuboresha utendaji na kusimamia maendeleo ya Zanzibar katika nyanja za kijamii, kiuchumi, kisiasa na kidiplomasia. Hongera sana, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi.

**7. Mheshimiwa Spika,** ninapenda nichukue fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.) kwa hotuba yake aliyoiwasilisha hapa Bungeni ambayo imetoa dira na mwongozo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali katika mwaka ujao wa fedha. Aidha, nampongeza kwa kuendelea kusimamia na kuratibu utendaji kazi na uwajibikaji Serikalini ambapo ufuatiliaji wake umetoa mwangwi wa uwajibikaji katika Utumishi wa Umma. Vilevile, namshukuru na kumpongeza kwa namna anavyotusimamia sisi mawaziri katika kutekeleza majukumu yetu.

**8. Mheshimiwa Spika,** sitoacha kukupongeza na kukushukuru kwa dhati wewe binafsi, Naibu Spika Mhe. Daniel Baran Sillo (Mb.), Wenyeviti wa Bunge, Wenyeviti wote wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge pamoja na watendaji wote wa Ofisi yako kwa namna mnavyolisimamia na kuliendesha Bunge letu tukufu kwa weledi na umahiri mkubwa. Juhudi na maarifa yenu yameendelea kuupa heshima Muhimili huu muhimu mbele ya umma wa watanzania na kuwezesha kuisimamia na kuishauri Serikali ipasavyo.

Aidha, ninawapongeza waheshimiwa wabunge wote kwa ujumla kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuwawakilisha wananchi katika Bunge hili fanyeni kazi Tanzania inatutegemea.

**9. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha tangu Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, Bunge lako tukufu limewapoteza wawakilishi wenzetu watatu ambao ni Mhe. Jenista Joakim Mhagama aliyekuwa mbunge wa jimbo la Peramiho, Mhe. William Vangimembe Lukuvi, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Isimani, mkoani Iringa, na Mhe. Halima Idd Nassor, aliyekuwa Mbunge Viti Maalum, Dar es Salaam. Kutokana na matukio hayo, naungana na wabunge wenzangu kutoa pole kwa Bunge lako tukufu, familia za marehemu, ndugu, jamaa, marafiki na wote walioguswa na misiba hiyo. Vilevile, niwatie moyo na kutoa pole kwa waheshimiwa wabunge na wananchi wote waliofiwa na ndugu na wapendwa wao kutokana na maradhi, ajali, majanga na matukio mbalimbali yaliyotokea katika nchi yetu. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina!

**10. Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Mhe. Msomi Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Songea Mjini, Makamu Mwenyekiti Mhe. Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe na Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/26 na Mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2026/27. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa katika bajeti hii.

**1955 - 2026**



### MHE. WILLIAM VANGIMEMBE LUKUVI

ALIYEKUWA MBUNGE WA JIMBO LA ISIMANI

**1967 - 2025**



### MHE. JENISTA JOAKIM MHAGAMA

ALIYEKUWA MBUNGE WA JIMBO LA PERAMIHO

**1983 - 2026**



### MHE. HALIMA IDD NASSOR

ALIYEKUWA MBUNGE VITI MAALUM

**11. Mheshimiwa Spika,** siwezi kuhitimisha salamu hizi za shukrani bila kumshukuru Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray (Mb.) kwa jinsi anavyonisaidia kwa karibu katika kutekeleza majukumu ya Ofisi yetu kwa uhodari na umakini mkubwa. Mhe. Naibu huyu, amefanya kazi yangu ya usimamizi kuwa nyepesi sana. Bungeni amejibu maswali kifasaha na ufahamu wake wa Wizara na kazi unamfanya kuwa Naibu Waziri wa kipekee. Ninakushukuru sana Naibu wangu. Asante Sana.

**12. Mheshimiwa Spika,** namshukuru Balozi Dkt. Moses M. Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi. Pia, nawashukuru Makatibu Wakuu, Bw. Mululi M. Mahendeka, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu; Bw. Juma S. Mkomi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Aidha, namshukuru Bw. Xavier M. Daudi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

**13. Mheshimiwa Spika,** vilevile, nawashukuru Makamishna, Watendaji Wakuu wa Taasisi; Wakurugenzi na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kutekeleza majukumu yanayoiwezesha Ofisi kufikia malengo yake, ikiwa ni pamoja na kukamilisha Hotuba hii kwa wakati. Aidha, napenda kuwashukuru waajiri na watumishi wa umma wote kwa kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi, uzalendo pamoja na imani yao kwa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita. Utendaji wao umeiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi.

**14. Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kuzishukuru Nchi Wahisani na Washirika wa Maendeleo ambao wamechangia jitihada zetu za kuleta maendeleo kwa wananchi. Hivyo, nachukua fursa hii kuwashukuru na niruhusu kuwataja wachache ambao ni:- Jamhuri ya Watu wa China, Japan, Uingereza, India, Jamhuri ya Korea, Canada, Marekani, Sweden, Ufaransa, Australia, Umoja wa Ulaya, Denmark, Norway, Uholanzi, Finland, Uswisi, Italia, Malaysia, Misri, Singapore, Cuba na Thailand. Vile vile, nayashukuru Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa ambayo ni: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), AU, SADC, OFID-OPEC Fund for International Development, FCDO, KOICA, GIZ, USAID, Indian Ocean Rim Association (IORA), EAC, Lake Victoria Basin Commission (LVBC) SIDA, UNDP, Jumuiya ya Madola, DANIDA, JICA, UNICEF, ILO, WFP, UN Women na Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF).

**15. Mheshimiwa Spika,** kwa umuhimu wa pekee kabisa ninawashukuru sana wananchi wenzangu wa Jimbo la Chalinze kwa kuendelea kuwa na imani na mimi na kunipa ushirikiano wakati wa utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, napenda kuishukuru familia yangu ikiongozwa na mke wangu, mama Aziza, na watoto wangu kwa kunipa ushirikiano, kuniombea na kuwa wavumilivu katika kipindi chote ninapokuwa katika kutekeleza majukumu ya kitaifa.

**16. Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kuwasilisha Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/27.

# MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/26

**17. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina mafungu saba (07) ya kibajeti ambayo ni: Ofisi ya Rais, Ikulu (Fungu 20 na 30); Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33); Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (Fungu 32); Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67); Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94); na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa (Fungu 04). Utekelezaji wa majukumu kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:-

## OFISI YA RAIS - IKULU NA TAASISI ZAKE

### A. Ofisi ya Rais - Ikulu

**18. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/26, Fungu: 20 Ofisi ya Rais, Ikulu iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 34,804,735,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **shilingi 26,131,358,572.70** sawa na **asilimia 75.08** zilipokelewa na kutumika.

**19. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu ya mwaka 2025/26, Fungu 30 Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri inayojumuisha taasisi zilizo chini ya Ikulu, iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 1,197,312,759,000.00**.

Kati ya fedha hizo **shilingi 1,039,839,675,000.00** sawa na **asilimia 86.74** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 157,473,084,000.00** sawa na **asilimia 13.26** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**20. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2026 **shilingi 854,951,739,283.67** sawa na **asilimia 71.41** zilipokelewa na kutumika ambapo **shilingi 773,197,434,626.00** ni Matumizi ya Kawaida na **shilingi 81,754,304,657.67** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**21. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hicho, Ofisi ya Rais, Ikulu ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Ushauri umetolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala ya Siasa, Uchumi, Jamii, Sheria, Diplomasia, Mawasiliano na Habari, Uhusiano wa Kikanda, Kimataifa na masuala mengine muhimu kwa lengo la kumsaidia Rais kufanya maamuzi;

(ii) Utekelezaji wa ratiba ya kila siku ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umewezeshwa;

(iii) Huduma zimetolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na familia yake;

(iv) Mikutano miwili (2) ya Baraza la Mawaziri imefanyika ambapo nyaraka 10 zimejadiliwa na kutolewa uamuzi. Mkutano wa Faragha (Retreat) wa Mwaka 2025/26 wa Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa na Naibu Makatibu Wakuu umefanyika ambapo ajenda mbili (2) zimejadiliwa; na Kikao kimoja (1) cha Wakuu wa Mikoa kimefanyika ambapo ajenda nane (8) zimejadiliwa;

1


IKULU, TUNGUU
TAIDEN
Mhe. Dkt. S. S. Hassan
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania







1 - 3: Kikao cha Baraza la Mawaziri cha tarehe 7 Januari 2026, kikiongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Ikulu Ndogo ya Tunguu, Zanzibar.

(v) Mikutano mitano (5) ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) imefanyika na nyaraka 15 zimechambuliwa na ushauri kutolewa. Aidha, mikutano ya kazi saba (7) ya Makatibu Wakuu imefanyika ambapo mada 22 zimewasilishwa na kujadiliwa;

(vi) Mikutano 11 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri imefanyika ambapo nyaraka 26 zimechambuliwa na kutolewa maoni na ushauri. Aidha, mikutano ya kazi minne (4) ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri imefanyika ambapo taarifa tisa (9) zimejadiliwa na kutolewa maoni na ushauri;

(vii) Kumbukumbu za Mikutano ya Baraza la Mawaziri, Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri zimeandaliwa na kusambazwa kwa wahusika kwa rejea na hatua za utekelezaji. Aidha, ufuatiliaji na tathmini ya maamuzi ya Baraza la Mawaziri umefanyika na taarifa imeandaliwa;

(viii) Mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Baraza la Mawaziri (e-Cabinet) kwa Mawaziri, Makatibu Wakuu, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Maafisa Uhusiano wa Baraza la Mawaziri (CLOs) waliokuwa wakiteuliwa yamefanyika kadri mahitaji yalivyokuwa yakijitokeza;

(ix) Mkutano mmoja (1) wa mafunzo ya Mwongozo wa Uandishi wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri wa Mwaka 2024 baina ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Maafisa Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri (CLOs) umefanyika;

(x) Mafunzo kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Nne (NACSAP IV) yamefanyika kwa washiriki 3,796 wakiwemo Wajumbe wa Kamati za Uadilifu, Watumishi na Viongozi kutoka katika taasisi 20 za umma na taasisi binafsi 870;

(xi) Taasisi za Umma zimeendelea kujengewa uwezo kupitia mafunzo mbalimbali ya uzingatiaji wa masuala ya utawala bora ambapo wajumbe 630 wa Kamati za Uadilifu wakiwemo (Wenyeviti na Makatibu) na Maafisa TEHAMA kutoka katika Sekretarieti za Mikoa 26 pamoja na Halmashauri zake 184 wamepatiwa mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Masuala ya Utawala Bora na Maboresho katika Sekta ya Umma "e-Maboresho";

(xii) Taarifa jumuishi za utekelezaji wa programu za Maboresho ikiwemo Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Nne katika vipindi vya robo ya kwanza na ya pili kwa mwaka 2025/26 zimeandaliwa na kuwasilishwa kwenye Mamlaka;

(xiii) Rufaa 297 za watumishi zimepokelewa na kati ya rufaa hizo rufaa 107, zimechambuliwa na kutolewa uamuzi. Aidha, malalamiko 265 yamepokelewa, kuchambuliwa na kutolewa uamuzi/maelekezo;

(xiv) Ujenzi wa jengo la makazi katika Ikulu Ndogo Arusha, ujenzi wa uzio kuzunguka jengo la Ofisi Chamwino na ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la Mapokezi Chamwino umekamilika;

(xv) Ujenzi wa jengo la Ofisi (Samia Building) katika Ikulu ya Chamwino Dodoma umefikia asilimia 63; na

(xvi) Ukarabati wa jengo la Ofisi na ujenzi wa majengo saidizi katika Ikulu ya Dar es Salaam umefikia asilimia 51.

## B. Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)

**22. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kutokomeza rushwa nchini; TAKUKURU imejiimarisha zaidi kwenye kuzuia vitendo vya rushwa kabla havijatokea.

**23. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026, TAKUKURU imetekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo 885 yenye thamani ya shilingi 599,629,035,456.12umefanyika ambapo miradi 13 yenye thamani ya shilingi 1,324,178,790.60 imebainika kuwa na kasoro mbalimbali na hatua zilizochukuliwa ni kutoa elimu kwa watekelezaji wa miradi kuhusu namna bora ya kusimamia miradi hiyo;

(ii) Uchambuzi wa mifumo 367 umefanyika kwa lengo la kubaini mianya ya rushwa katika utoaji wa huduma za jamii ikiwemo afya, elimu, maji, ujenzi, fedha, mawasiliano, utawala, mafuta na gesi, biashara, umeme, kilimo, madini na usafirishaji. Kutokana na chambuzi hizi mapendekezo ya kuziba mianya ya rushwa yalitolewa;

(iii) Vikao kazi 242 vya wadau na kazi 133 za ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikakati ya kuziba mianya ya rushwa iliyobainishwa katika matokeo ya kazi za utafiti, uchambuzi wa mifumo na ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma katika miradi ya maendeleo zimefanyika;

(iv) Kushiriki kongamano la maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika la tarehe 11 Julai, 2025 na kujadili mafanikio na changamoto za mapambano dhidi ya rushwa ili kuimarisha juhudi za pamoja katika kuitokomeza;

(v) Kushirikiana na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) kuandaa maudhui kuhusu kuzuia na kupambana na rushwa yatakayojumuishwa katika somo la 'Historia ya Tanzania na Maadili' kwa darasa la sita na kidato cha nne. Aidha, maudhui haya yamejumuishwa katika somo hili kwa darasa la tatu, la nne, la tano na la sita kwa shule za msingi; na kidato cha kwanza, cha pili, cha tatu na cha tano katika shule za sekondari;

(vi) Kufungua klabu mpya za wapinga rushwa 176 na kuimarisha Klabu 4,813 katika shule za msingi na sekondari;

(vii) Kuwashirikisha na kuwaelimisha wadau mbalimbali kuhusu haki na wajibu wao katika mapambano dhidi ya rushwa ikiwemo kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kupitia semina 3,393, mikutano ya hadhara na mijadala ya wazi 2,710 na kushiriki maonesho 306;







1. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akipokea Taarifa ya Mwaka ya Utendaji kazi wa TAKUKURU katika hafla iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam.
2. Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Bw. Crispin Chalamila akiwasilisha taarifa ya mwaka ya utendaji kazi wa TAKUKURU kwa Mheshimiwa Rais katika hafla iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam.

(viii) TAKUKURU imeendelea kushirikiana na vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kuhabarisha na kuelimisha kuhusu mapambano dhidi ya rushwa, ambapo vipindi 431 vya redio na televisheni vimerushwa, makala za video 107 zimeandaliwa na kurushwa kupitia televisheni mtandao ya TAKUKURU TV. Vilevile, matangazo (graphic adverts) 19yameandaliwa na kusambazwa kupitia vituo vya redio, televisheni na mitandao ya kijamii;

(ix) Uelimishaji kuhusu umuhimu wa kusimamia miradi ya maendeleo na kushiriki uchaguzi Mkuu pasipo kujihusisha na vitendo vya rushwa wakati wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2025 umefanyika katika halmashauri zote za Tanzania Bara;

(x) Katika kipindi cha Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, TAKUKURU iliandaa matangazo sita (6) ambapo matangazo manne (4) yalisambazwa kupitia *billboards* katika majiji yote nchini na matangazo mawili (2) yalisambazwa kupitia runinga (TV) ya treni inayotumia reli ya SGR. Aidha, TAKUKURU kupitia huduma ya bulk SMS ilisambaza ujumbe wa kuhamasisha wananchi kuzuia vitendo vya rushwa katika uchaguzi;

(xi) TAKUKURU iliendesha semina kwa viongozi wa dini, wahariri wa vyombo vya habari, wadau wa taasisi zisizo za kiserikali na asasi za kiraia na wajumbe wa Baraza la Vyama vya Siasa ili kuimarisha ushiriki wao katika kudhibiti vitendo vya rushwa katika uchaguzi, kwaya ya TAKUKURU iliandaa nyimbo mbili zinazohamasisha wananchi kuzuia na kupambana na vitendo vya rushwa katika uchaguzi ambazo zilisambazwa kupitia TAKUKURU TV;

(xii) Kesi 664 zimeendeshwa mahakamani zikiwemo kesi mpya 305. Kati ya kesi mpya zilizofunguliwa mahakamani 3 ni kesi kubwa ambazo zimefunguliwa katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi. Kesi 325 zimeamuliwa mahakamani ambapo Jamhuri ilishinda kesi 260 kwa watuhumiwa kuhukumiwa kifungo au/na kulipa faini. Hadi kufikia Machi, 2026 kesi 339 zinaendelea mahakamani;

(xiii) Kiasi cha shilingi 102,358,636,166.00 zimeokolewa kutokana na operesheni mbalimbali za uchunguzi uliofanyika kote nchini ambapo shilingi 85,153,488,589.00 ni fedha taslimu zilizorejeshwa Serikalini na shilingi 17,205,147,577.00 zimedhibitiwa na kurejeshwa katika miradi mbalimbali ya Serikali na kwa walalamikaji wa Sekta binafsi;

(xiv) Ujenzi wa jengo la Ofisi ya TAKUKURU Makao Makuu umefikia asimilia 92; Ofisi za Mkoa wa Morogoro (90%) na Singida (36%); Ofisi za wilaya ya Ludewa (69.6%), Kwimba (70.6%), Hai (75.8%), Mlele (90.7%), Tandahimba (59.1%), Nachingwea (74.3%) na Karatu (65.3%); na nyumba za makazi za watumishi katika wilaya ya Momba (50%). Aidha, ujenzi wa Ofisi katika wilaya za Pangani, Kondoa na Kyerwa uko katika hatua za awali;

(xv) Ofisi 12 za Wilaya zimeunganishwa na mtandao wa ndani wa TAKUKURU; Buhigwe, Bunda, Kaliua, Malinyi, Kilindi, Mafia, Makete, Mbulu, Ngara, Nyang’hwale, Rungwe na Ukerewe; na

(xvi) Shughuli za ukarabati wa mtandao katika Ofisi ya Ilemela na Upanga; kusanikisha mtandao katika Ofisi ya TAKUKURU Longido na kufanya ukaguzi wa mtandao na CCTV kamera Ofisi ya TAKUKURU Arusha, Bukoba na Meatu zimekamilika.




1. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Kamati hiyo mara baada ya kutembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa jengo la TAKUKURU, Wilaya ya Nyang'wale, Mkoani Geita.

## C. Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

**24. Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF umeendelea kutekeleza Awamu ya Tatu ya TASAF kwa kuweka kipaumbele kwenye maeneo ya Ukuzaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato; Kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii; na Utawala bora na uwajibikaji.

**25. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026; Mfuko wa Maendeleo Jamii - TASAF umetekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Ruzuku ya Serikali ya jumla ya shilingi 43,531,884,398 ilihawilishwa kwa Kaya za Walengwa 896,746 katika maeneo 186 ya utekelezaji. Aidha, Walengwa 535,536 sawa na asilimia 60 ya kaya zote zimesajiliwa na kupokea ruzuku kwa njia ya kielektroniki kupitia mitandao ya simu na akaunti za benki;

(ii) Miradi 98 ya kijamii imetekelezwa ambapo Kaya za Walengwa 226,010 zimeshiriki kufanya kazi za ajira za muda katika sekta za afya, elimu na maji;

(iii) Miradi 78 ya uendelezaji wa miundombinu yenye thamani ya shilingi 2,880,000,000.00 imepatiwa fedha na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji;

(iv) Uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA ili kuendana na Muundo wa Mpango unaofuata wa Kunusuru Kaya Maskini Awamu ya III na utekelezaji wa Sera ya Kinga ya Jamii umefanyika. Kazi hii imehusisha kufanya mapitio kwa ajili ya maboresho makubwa yanayoendana na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya taarifa za walengwa kwa taasisi na wadau wengine;

(v) Uchakataji na uchambuzi wa data za tathmini ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Awamu ya III umekamilika na matokeo ya awali yamewasilishwa kwa wadau. Baadhi ya mapendekezo yametumika kuboresha usanifu wa Mpango unaofuata hususan utekelezaji wa afua za ruzuku ya uzalishaji mali na miradi ya ajira za muda;

(vi) Mpango awamu inayofuata (PSSN III) unaotarajiwa kugharimu takribani dola za Marekani milioni 300 na kutekelezwa kwa miaka minne (4) kuanzia mwaka 2026 hadi 2029 umeidhinishwa rasmi na Bodi ya Benki ya Dunia tarehe 31 Machi 2026; na

(vii) TASAF imekamilisha maandalizi ya zoezi la utambuzi na uandikishaji wa Walengwa wa Mpango unaofuata ikiwemo maboresho ya mifumo ya TEHAMA na Miongozo ya zoezi la utambuzi. Zoezi la utambuzi litaanza baada ya Mpango kuidhinishwa na Benki ya Dunia.







1. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete (kulia) akifurahia jambo na Mkurugenzi wa TASAF, Bw. Shadrack Mziray (kushoto) wakati wa ziara ya kikazi ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria iliyolenga kukagua utekelezaji wa mradi wa Zahanati ya Mihama uliotekelezwa na TASAF iliyopo Kata ya Kitangiri, Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela, Mkoani Mwanza.

## D. Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)

**26. Mheshimiwa Spika,** kutokana na kuimarika kwa matumizi ya TEHAMA katika Taasisi za Umma, Serikali ya Tanzania imetambulika Kimataifa katika matumizi ya TEHAMA Serikalini kupitia Mfumo wa e-Mrejesho toleo la pili (e-Mrejesho v2) ambao unawawezesha wananchi kuwasiliana na viongozi kuanzia ngazi ya Waziri, Wakuu wa Mikoa na Wilaya. Kupitia Mfumo huu, Tanzania ilishinda Tuzo za Mkutano wa Dunia wa Jumuiya ya TEHAMA mwaka 2025 (World Summit on the Information Society - WSIS 2025 Grand Champion) katika kipengele cha Serikali Mtandao iliyofanyika Geneva, Uswisi Julai, 2025.Tuzo hizo ambazo huratibiwa na Shirika la Mawasiliano la Umoja wa Mataifa (International Telecommunications Union – ITU), zinalenga kutambua na kuchochea kazi au miradi bunifu inayotumia TEHAMA katika kuchangia maendeleo endelevu duniani.

Aidha, Serikali ya Tanzania imeorodheshwa katika Kundi A - Ukomavu wa Juu wa matumizi ya TEHAMA (Extensive GovTech Maturity), kupitia Ripoti ya Utafiti ya Benki ya Dunia iliyotolewa Disemba, 2025 kuhusu Ukomavu wa Matumizi ya Teknolojia Duniani katika Utoaji wa Huduma za Serikali na Ushirikishwaji wa Wananchi - GovTech Maturity Index (GTMI).

**27. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Serikali Mtandao imeendelea kuimarisha na kuendeleza utoaji wa huduma za Serikali Mtandao kwa taasisi za umma kwa kutekeleza afua mbalimbali zinazolenga kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

**28. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026 shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:

(i) Uboreshaji wa miundombinu ya kuhifadhi mifumo shirikishi ya Serikali Mtandao ambapo ununuzi wa seva za kuhifadhi data na vifaa vingine umefanyika, hatua iliyoongeza uwezo na usalama wa uhifadhi wa taarifa katika vituo husika;

(ii) Uhuishaji wa miundombinu ya vituo vya kuhifadhi data na taarifa umefanyika kwa kununua vifaa vya TEHAMA, kuboresha mfumo wa umeme wa dharura (power backup), kununua vifaa vya miundombinu ya kangavuke (generator) kwa ajili ya kuwezesha mifumo ya kiotomatiki kufanya kazi na ununuzi wa vifaa vya Kituo cha Kusimamia Uendeshaji wa Miundombinu ya Serikali Mtandao (Network Operations Centre - NOC), vikiwemo leseni ya SolarWinds na SmartNet ili kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa miundombinu ya TEHAMA;

(iii) Tathmini ya usalama imefanyika kwa mifumo 355 inayopatikana mtandaoni kati ya mifumo 450 iliyopangwa kufanyiwa tathmini. Aidha, tathmini ya uzingatiaji wa viwango na miongozo ya usalama wa Serikali Mtandao imefanyika katika taasisi 91 kati ya taasisi 150 zilizopangwa kufanyiwa tathmini kwa lengo la kuhakikisha kuwa mifumo na miundombinu ya TEHAMA Serikalini inafanya kazi kwa ufanisi, na kutoa huduma bora, salama, na endelevu kwa wananchi;

(iv) Kusimamia, kuendesha na kuendeleza mifumo na miundombinu shirikishi ya TEHAMA ya Serikali na taasisi zake, ikiwa ni pamoja na mifumo ya TEHAMA na mtandao wa mawasiliano serikalini ikiwemo kusimamia na kuboresha vituo vya kuhifadhi mifumo ya Serikali na vituo vya kujikinga na majanga;

(v) Tafiti mbili (2) zilifanywa kwenye maeneo ya Udhibiti wa Uboreshaji wa Usimamizi wa Rekodi za Kielektroniki katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali (MDAs) na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) nchini; na Uundaji wa Muundo wa Kujifunza kwa Mashine ya Honeypot kwa ajili ya kugundua programu hasidi katika Mitandao. Applications nne za uvumbuzi (msaadaai.all.tz, sentiment.all.tz, Sentiment mobile application, Signature attendance Stamp (SAS)) ziliwezeshwa;

(vi) Kusanifu na kujenga mifumo minne (4) mipya (TMA-MIS, AQRB-MIS, AICC Event & Estate MIS na Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Wafungwa (PIMIS);

(vii) Kuboresha usalama wa watumiaji wa vifaa vya TEHAMA serikalini kwa kusanifu na kujenga mfumo wa NGAO wa kitaifa ili kuongeza usalama wa mifumo ya TEHAMA serikalini ambapo taasisi na vituo vya kutolea huduma 538 vimejiunga na mfumo huo na kufanya jumla ya taasisi na vituo vya kutolea huduma kufikia 723. Lengo ni kuhakikisha Taasisi zote 780 zinazotumia Mfumo wa Baruapepe (Goverment Mailing System- GMS) zinajiunga na Mfumo wa NGAO;

(viii) Uunganishaji wa mifumo ya TEHAMA katika Mfumo wa Pamoja wa Ubadilishanaji wa Taarifa Serikalini (Government Enterprise Service Bus, GovESB) unaowezesha mifumo ya TEHAMA ya Serikali kubadilishana taarifa umefanyika, ambapo mifumo mikuu iliunganishwa na inabadilishana taarifa ikiwemo mifumo ya Taasisi za Sekta ya Haki Jinai ya Mahakama, TAKUKURU, POLISI na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka. Hadi kufikia Machi, 2026 mifumo mipya 28 imeunganishwa kwenye Mfumo wa kubadilishana taarifa na kufanya jumla ya mifumo iliyounganishwa kufikia 252 kutoka taasisi 200 za Serikali;

(ix) Kuunganisha taasisi mpya na vituo vya kutolea huduma 328 kwenye Mfumo wa Saini za kidijitali na kufanya jumla ya taasisi za umma na vituo vya kutolea huduma vilivyounganishwa kufikia 528 kati ya taasisi na vituo 780 zinazotumia Mfumo wa Baruapepe Serikalini. Aidha, taasisi mpya 46 zimeunganishwa kwenye Mfumo wa Ofisi Mtandao na kufanya jumla ya taasisi zilizounganishwa kufikia 425 kati ya taasisi 571;

(x) Kuhuisha na kufanya maboresho katika Mifumo ya TEHAMA shirikishi, Mifumo ya Kisekta na Kitaasisi inayotumika kuziwezesha kuboresha utoaji huduma katika Utumishi wa umma na kwa wananchi ikiwemo mifumo ya e-Office, GMS, ERMS, e-Board, e-Mrejesho V2, e-Ukaguzi, na e-Mikutano;

(xi) Kuongeza wigo wa Mtandao wa Mawasiliano Serikalini kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali, ambapo taasisi na vituo vya kutolea huduma 660 zinaunganishwa kwenye Government Networkkupitia Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa kwenye Wilaya mbalimbali nchini;

(xii) Tathmini ya uzingatiaji wa viwango na miongozo ya Serikali Mtandao imefanyika kwa Taasisi za Umma 91 kati ya 150 zilizopangwa kufanyika;

(xiii) Ukaguzi wa mifumo 64 ya kimkakati ya TEHAMA kutoka katika Taasisi za Umma za kisekta na kitaasisi umefanyika;

(xiv) Mafunzo ya usalama TEHAMA kwa njia nadharia na vitendo yametolewa kwa wataalamu wa TEHAMA wa taasisi za Umma 126 kati ya 160 zilizopangwa kupatiwa mafunzo, na elimu ya usalama wa mtandao (Cyber security awareness) imetolewa kwa watumiaji wa mifumo ya TEHAMA kutoka taasisi za Umma 558 kati ya taasisi 571; na

(xv) Taasisi za umma 120 zimepatiwa huduma ya ushauri wa kitaalamu na msaada wa kiufundi kwenye maeneo ya TEHAMA.




1. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete, Viongozi mbalimbali pamoja na Washiriki wa mkutano wa sita wa Serikali Mtandao wakifuatilia jambo kwenye mkutano huo uliofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC), Arusha.

2




2. Washiriki wa mkutano wa sita wa Serikali Mtandao wakiwa kwenye mkutano huo uliofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC) jijini Arusha. Wengine ni Viongozi na Watendaji wa Taasisi mbalimbali.

## E. Taasisi ya UONGOZI

**29. Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Uongozi imeendelea kusimamia malengo yake ya kuwa Kituo cha utaalamu wa hali ya juu cha kuendeleza viongozi Barani Afrika kwa kuanzia na Tanzania, ukanda wa Afrika Mashariki na hatimaye Afrika kwa ujumla. Walengwa ni viongozi waandamizi waliopo na wanaojitokeza wakiwemo wanasiasa, watumishi wa Serikali na Mahakama.

**30. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwezi Julai, 2025 hadi Machi, 2026 shughuli zifuatazo zimetekelezwa: -

(i) Mafunzo ya Stashahada ya Uzamili ya Uongozi yametolewa kwa maafisa waandamizi 35 kutoka wizara, taasisi na mashirika ya umma, taasisi za kiraia na taasisi binafsi, ambapo moduli nane (8) zimetolewa kama ilivyopangwa. Moduli hizo zilihusu; Ujuzi wa Fedha kwa Wasimamizi, Kuongoza kwa Matokeo, Mbinu za Ubunifu kwa Maendeleo ya Shirika, Maendeleo Endelevu, Uongozi wa Kimaadili, Mawasiliano ya Kimkakati, Usimamizi wa Rasilimaliwatu Kimkakati na Uongozi Binafsi na wa Taasisi;

(ii) Mafunzo ya uongozi katika ngazi ya cheti yametolewa kwa njia ya mtandao kwa jumla ya viongozi 72, ambayo yalikuwa na moduli tano (5), zikihusu Misingi ya Ufahamu wa Kihisia, Misingi ya Kuongoza Mabadiliko, Matumizi ya Takwimu na Uchanganuzi katika Uongozi, Usimamizi wa Rasilimali Fedha na Mbinu za Ubunifu. Washiriki wa mafunzo walitoka katika wizara, taasisi na mashirika ya umma, asasi za kiraia pamoja na Taasisi Binafsi;

(iii) Mafunzo yenye moduli tano (5) kuhusu; uongozi kupitia akili hisia, upangaji wa kimkakati na taswira ya baadaye, uongozi wenye uwajibikaji, pamoja na ufanyaji wa maamuzi kwa msingi wa Ushahidi, yalitolewa kwa viongozi wanaochipukia 35 yakiwa na lengo la kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu ya uongozi. Programu imehusisha viongozi chipukizi kutoka Serikali Kuu, Taasisi za Umma, Mashirika Binafsi pamoja na Asasi za Kiraia;

(iv) Programu maalum kwa viongozi wanawake 100 kutoka Taasisi za Umma, Taasisi Binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ilitekelezwa kwa asilimia 100. Aidha, baadhi ya washiriki walitoka nje ya nchi, zikiwemo Afrika Kusini, Zambia, Rwanda, Kenya, Uganda, Namibia, Nigeria, Ethiopia, Botswana, Lesotho, Zimbabwe, Eswatini, Cameroon na Gambia. Programu hii ilijumuisha moduli 24 zilizolenga kuchangia jitihada za kitaifa katika kushughulikia changamoto ya uwakilishi mdogo wa wanawake katika nafasi za juu za maamuzi serikalini, katika siasa, biashara na taasisi za kiraia;

(v) Kozi 33 za muda mfupi, zimetolewa kwa viongozi 1,433, miongoni mwa viongozi hao, 104 ni wakuu wa taasisi na mashirika ya umma. Kozi hizo, zililenga kuwajengea uwezo binafsi katika maeneo mbalimbali yakiwemo; Ufahamu wa Kihisia, Uongozi Binafsi, Uongozi wa Rasilimali za Umma, Utawala Bora na Mbinu za Uwakilishi wa Uongozi na Uongozi wa Timu zenye Utendaji wa Juu;

(vi) Mafunzo 25 ya uongozi yametolewa kwa wakurugenzi 514 wa bodi za wakurugenzi wa taasisi na mashirika ya umma kuhusu; Uongozi wa Kimkakati, Usimamizi wa Mashirika ya Umma, Usimamizi wa Rasilimali za Umma, Rasilimaliwatu na Usimamizi wa Viashiria Hatarishi;

(vii) Tafiti tumizi mbili (2) zinazohusu Kujenga Uendelezaji wa Uongozi nchini Tanzania (mtazamo wa kihistoria kuelekea mabadiliko) na Maendeleo ya Uchumi wa Maeneo nchini Tanzania zimekamilika;

(viii) Uandishi wa tawasifu ya Hayati Rashid Mfaume Kawawa, aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umeendelezwa, ambapo sura za awali zimeshawasilishwa na kwa sasa zinapitiwa ili kuhakikisha ubora kabla ya kuendelea na uandishi wa sura zilizobaki. Aidha, zoezi la ukusanyaji wa taarifa kwa ajili ya maandalizi ya uandishi wa tawasifu ya Hayati Rais wa Zanzibar, Abeid Amani Karume linaendelea;

(ix) Makongamano matatu (3) ya kitaifa na moja (1) la kikanda yaliandaliwa kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za ndani ya nchi ambapo viongozi 430 walishiriki. Makongamano hayo ni: Kongamano la Kikanda kuhusu Mchango wa Wanawake katika Uongozi Barani Afrika; Mkutano wa Kitaifa kuhusu Maendeleo ya Uchumi wa Ndani; na Kongamano la Kitaifa kwa Wataalamu wa Uchumi, Biashara na Sekta ya Fedha na Jukwaa la Maendeleo Endelevu lililolenga kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa maendeleo endelevu; na

(x) Machapisho nane (8) juu ya masuala ya uongozi na maendeleo endelevu yamefanyika. Kati ya hizo nne (4) ni ripoti za tafiti na nne (4) za muhtsari wa sera.




1. Mhe. Bal. Dkt. Moses Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akifungua mafunzo ya uongozi wa viongozi wakuu wa taasisi na mashirika ya umma Julai 2025.

1


Emerging Leaders Programme
SUOMI FINLAND
UONGOZI Institute
Emerging Leaders Programme
Supporting rising leaders to grow and thrive
11 December, 2025 | Dar es Salaam
Emerging Leaders Programme
11 December, 2025 | Dar es Salaam

2


Institute
Funded by the European Union
UN WOMEN
LEADERSHIP PROGRAMME
ADVANCING WOMEN INTO LEADERSHIP ROLES




1. Mhe. Regina Ndege Qwaray (Mb.), Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, akizindua Programu ya Viongozi Chipukizi (*Emerging Leaders Programme*) Desemba 2025, Dar es Salaam.
2. Majadiliano wakati wa vipindi vya darasani vya Programu ya Uongozi kwa Wanawake Oktoba 2027. Utekelezaji wa Programu hii unawezeshwa kwa kiasi kikubwa na Serikali ya Tanzania, Serikali ya Finland, na Umoja wa Ulaya.
3. Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, akiwasilisha mada wakati wa mafunzo ya uongozi wa viongozi wakuu wa taasisi na mashirika ya umma Julai 2025.

## F. Wakala wa Ndege za Serikali

**31. Mheshimiwa Spika,** Wakala ya Ndege za Serikali Tanzania ina jukumu la kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Viongozi wengine Wakuu wa Kitaifa. Wakala ilianzishwa ili kuboresha huduma na kuimarisha usalama wa usafiri wa ndege kwa Viongozi wanaotumia huduma hizo. Aidha, Wakala imeongezewa jukumu lingine la kuratibu kwa niaba ya Serikali, ununuzi wa ndege, kuzikodisha kwa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) na kusimamia mikataba ya ukodishwaji wa ndege hizo.

**32. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 shughuli zifuatazo zimetekelezwa: -

(i) Huduma ya usafiri wa anga imeendelea kutolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Viongozi wengine Wakuu wa Kitaifa;

(ii) Gharama za bima za ndege pamoja na bima za Wanaanga zimelipwa;

(iii) Wanaanga 30 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi ili kuhuisha leseni zao;

(iv) Matengenezo ya ndege Fokker 50 yamefanyika kwa mujibu wa kalenda ya mtengenezaji; na

(v) Ukarabati na upanuzi wa Karakana ya Ndege za Serikali iliyopo katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere - Terminal I unaendelea na umefikia asilimia 96.

## G. Baraza la Kumshauri Rais Kuhusu Masuala ya Chakula na Kilimo

**33. Mheshimiwa Spika,** Baraza la Kumshauri Rais kuhusu Masuala ya Kilimo na Chakula linajukumu la kumshauri Rais kuhusu masuala mbalimbali yahusuyo chakula na kilimo.

**34. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, shughuli zilizotekelezwa ni: -

(i) Mpango Mkakati wa Baraza wa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia mwaka 2026/27 hadi 2030/31 umeandaliwa na umeainisha malengo muhimu yanayohusu masuala ya chakula na kilimo;

(ii) Baraza kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo imetafuta rasilimali fedha ambapo dola za Marekani 398,840 kati ya dola za Marekani 1,000,000 kutoka Alliance for Green Revolution Africa (AGRA) zimepatikana katika awamu ya kwanza kwa ajili ya kusimamia uendelezaji wa sekta ya kilimo na kuimarisha ushiriki wa vijana katika kilimo;

(iii) Maandiko ya kisera kwenye maeneo mbalimbali yanayohusu kilimo na chakula yameandaliwa, ambayo ni: Andiko la Uwekezaji wa Mitaji katika Sekta ya Kilimo kutoka Sekta Binafsi; Andiko la Kuimarisha na Kuongeza Upatikanaji wa Huduma za Kifedha na Kidijitali; Andiko la Mbinu Bora za Kimataifa za Mabadiliko ya Kilimo; Andiko la Umuhimu wa Serikali Kuendeleza Mifumo yenye Tija katika Kusimamia na Kuendeleza Mnyororo wa Thamani ya Mazao na Bidhaa za Chakula na Kilimo; na maandiko mengine ya kisera katika maeneo 11 ya kimkakati kutoka kwenye Mwongozo wa Marejeo katika Mpango wa Utekelezaji wa Masuala ya Chakula;

(iv) Mikutano ya Jukwaa la Kimataifa la Masuala ya Mifumo ya Chakula Afrika (Africa Food Systems Forum - AFSF) iliyofanyika Dakar, Senegal na katika Jukwaa la Chakula Duniani (World Food Forum) Roma, Italia imehudhuriwa. Pamoja na masuala mengine, majukwaa haya yamesaidia kujenga uelewa zaidi na kupata uzoefu wa nchi nyingine kuhusu masuala mbalimbali ikiwemo hatua zilizofikiwa na nchi kwenye uendelezaji wa mifumo ya chakula, ushiriki wa vijana na matumizi ya teknolojia ya kisasa katika sekta ya kilimo; na

(v) Mikutano miwili (2) ilifanyika na kutanisha wadau 613 kutoka sekta za kilimo, mifugo na uvuvi, ambapo wadau 273 ni kutoka Kanda ya Kati ikihusisha Mikoa ya Dodoma, Manyara na Singida na wadau 340 kutoka Kanda ya Magharibi ikihusisha Mikoa ya Tabora, Kigoma na Katavi. Mikutano hii ni mwendelezo wa mikutano iliyofanyika katika Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Ziwa. Mikutano hii inatoa fursa kwa wadau wa kilimo, mifugo na uvuvi kujadili na kushauri nini kifanyike katika kufikia malengo ambayo Tanzania imejiwekea kufuatia maazimio ya Mkutano wa Kilele (Summit) iliofanyika Dakar, Senegal mwezi Januari 2023 kuhusu Afrika kujitosheleza kwa chakula.




1. Baraza la Kumshauri Rais kuhusu Masuala ya Kilimo na Chakula, likiongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Mizengo Pinda, Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lilipokutana kwa mazungumzo na Viongozi wa Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi Machi 2026, Dodoma.

## FUNGU 33 - OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

**35. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2025/26, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 16,958,139,000.00**. Kati ya fedha hizo **shilingi13,958,139,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sawa na **asilimia 82.31** na **shilingi 3,000,000,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na a**silimia 17.69**.

**36. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi, 2026 fedha kiasi cha **shilingi 10,817,581,564.81** sawa na **asilimia 63.79** ya bajeti iliyoidhinishwa kilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo **shilingi 10,439,378,502.81** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 378,203,062.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**37. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2025/26, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imetekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Jumla ya matamko ya Rasilimali na Madeni ya viongozi wa umma 15,034 kati ya 17,742 sawa na asilimia 85 yamepokelewa kupitia Njia ya Mtandao (Online Declaration System) hadi kufikia muda wa mwisho wa urejeshaji. Kati ya matamko yaliyopokelewa, Matamko ya mwaka yalikuwa 10,897, Cheo Kipya 3,980 na Matamko ya mwisho wa kutumikia wadhifa yalikuwa 157;

(ii) Malalamiko 120 ya ukiukwaji wa maadili dhidi ya viongozi wa Umma yalipokelewa na kuchambuliwa. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 92 yalihusu Sheria ya Maadili na Malalamiko 28 hayakuhusu Sheria, hivyo yaliwasilishwa kwa taasisi husika. Aidha, kwa malalamiko yanayohusu sheria, asilimia 19 uchunguzi umekamilika na asilimia 81 uchunguzi bado unaendelea;

(iii) Jumla ya Viongozi wa Umma 258 walifanyiwa uhakiki wa tamko la rasilimali na madeni na utambuzi wa mgongano wa maslahi. Matokeo ya uhakiki yanaonesha kuwa asilimia 16.3 ya viongozi walibainika kuwa na kasoro katika matamko ya Rasilimali na Madeni. Hatua mbalimbali zimechukuliwa kwa Viongozi waliobainika kuwa na kasoro ikijumuisha kurekebisha kasoro husika; kufanyiwa uchunguzi wa awali na baadhi kufikishwa kwenye Baraza la Maadili kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi wa kina;

(iv) Wadau 26,607 walipatiwa elimu ya maadili ambapo viongozi wa umma walikuwa ni 6,277, watumishi wa umma 15,987 na wananchi 7,343. Aidha, elimu ya maadili ilitolewa kupitia vyombo vya habari ambapo jumla ya vipindi 95 vya redio na viwili (2) vya runinga vilirushwa hewani;

(v) Jumla ya Klabu mpya za Maadili 170 zilianzishwa kutoka shule za Msingi 106 na Sekondari 64 zikiwa na wanachama zaidi ya 5,918. Vilevile, Klabu za Maadili 530zilitembelewa na maafisa wa Sekretarieti kwa lengo la kuziimarisha na kuwajengea uwezo wanachama. Kati ya Klabu zilizotembelewa, shule za Msingi zilikuwa ni 295,Sekondari 227 na Vyuo Nane (8) zikiwa na wanachama zaidi ya 25,853;

(vi) Jumla ya Viongozi 4,659 walisaini Hati ya Ahadi ya Uadilifu ambapo Viongozi wanaume ni asilimia 69 na wanawake ni asilimia 31;

(vii) Ujenzi wa jengo jipya la Ofisi za Makao Makuu Dodoma lililopo eneo la NCC Kilimani, Mtaa wa Maadili limekamilika na kutumika. Aidha, ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Kanda ya Ziwa (Mwanza) umefikia asilimia 41 na kwa upande wa ujenzi wa jengo la Kanda ya Mashariki (Morogoro) Mshauri Elekezi amepatikana na zabuni imetangazwa; na

(viii) Kikao kimoja (1) kwa ajili ya kusikiliza lalamiko moja (1) la Ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa uchunguzi wa kina kimefanyika.




1. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Kamati yake mara baada ya kukagua utekelezaji wa Mradi wa ujenzi wa Ofisi za Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma iliyopo Buswelu, Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela, Mkoani Mwanza. Kulia kwake ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-UTUMISHI na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete na kushoto kwake ni Kamshina wa Maadili Mhe. Jaji (Mst.) Sivangilwa Mwangesi.

## FUNGU 32 - OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA NA TAASISI ZAKE

**38. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa fedha 2025/26, Fungu 32, linalojumuisha Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC) na Watumishi Housing Investment (WHI) lilitengewa jumla ya **shilingi 74,842,329,000.00**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 55,086,788,000.00** sawa na **asilimia 73.60** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 19,755,541,000.00** sawa na **asilimia 26.40** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**39. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2026 kiasi cha **shilingi 48,723,686,945.20**, sawa na **asilimia 65.10** ya bajeti iliyoidhinishwa kilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo **shilingi 44,317,453,021.80** ni Matumizi ya Kawaida na **shilingi 4,406,233,923.40** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Yafuatayo ni maelezo ya matumizi kwa kila taasisi: -

### A. Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

**40. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na taasisi zake ilitekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Vibali vya ajira mpya 43,866 vimetolewa, ambapo nafasi 41,500 zimeidhinishwa kwa Taasisi zinazolipa mishahara kupitia Mfumo wa e-Watumishi na nafasi 2,366 zimeidhinishwa kwa Taasisi zinazolipa mishahara ya watumishi kupitia mapato ya ndani;

(ii) Madai ya malimbikizo ya mishahara kwa watumishi wa umma 13,551 yenye thamani ya shilingi 17,739,793,480.17 kwa watumishi kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi za Umma yamehakikiwa na kulipwa;

(iii) Madai ya malimbikizo ya mishahara kwa watumishi wa umma 1,241 waliokoma utumishi wao kwa sababu mbalimbali yenye thamani ya shilingi 5,533,991,113.38 kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, na Taasisi za Umma yamehakikiwa na kulipwa;

(iv) Taarifa 190,132 za kiutumishi na mishahara katika Orodha ya Malipo ya Mishahara (Payroll) zikiwemo taarifa za Ajira Mpya/Mbadala 45,482; Mabadiliko ya Hali ya Kiutumishi 1,287; Usafishaji wa Taarifa (Data Cleaning) 24,978; Mabadiliko ya Mishahara 2,449; Mshahara Binafsi 489; Uidhinishaji wa Posho 89,043; Kurejeshwa katika Utumishi wa Umma 1,523; Ubadilishwaji Kada 4,051; na Upandishwaji vyeo 20,830 zimechambuliwa na kuidhinishwa kupitia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (*e-Watumishi*);

(v) Uhakiki wa taarifa za watumishi 17,432 umefanyika katika Wizara ya Afya makao makuu, Hospitali za rufaa za Mikoa 28, Hospitali za Rufaa za Kanda tatu (3) na Hospitali maalum mbili (2);

(vi) Watumishi 18,300 wa kada na ngazi mbalimbali katika Sekretarieti za Mikoa 13 ya Pwani, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Njombe, Iringa, Morogoro, Songwe, Mbeya, Rukwa, Katavi, Kigoma na Tabora; na Mamlaka za Serikali za Mitaa 90 katika mikoa husika, wamejengewa uwezo na kutatua changamoto zinazokwamisha usimamizi wa utendaji kazi kupitia Mfumo wa e-Utendaji katika maeneo yao kupitia *“Mobile Clinic”*;

(vii) Vibali 611 vya kujaza nafasi za uongozi katika Taasisi za Umma, vibali 311 vya kukaimu nafasi mbalimbali za uongozi, vibali 1,345 vya ajira mbadala pamoja na vibali 707 vya likizo bila malipo vimetolewa. Aidha, vibali 5,469 vya uhamisho wa watumishi vimetolewa kwa lengo la kuboresha utendaji kazi katika Utumishi wa Umma;

(viii) Mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa e-Watumishi yametolewa kwa Maafisa Utumishi 291, Wakuu wa Idara za Utumishi na Utawala 20, Wakaguzi wa Ndani 56 na Wahasibu 72 wa Taasisi za Umma;

(ix) Mafunzo ya dirisha la e-Uhamisho yametolewa kwa Mamlaka mbili (2) za uhamisho ambazo ni Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI) na Makatibu Tawala wa Mikoa 26 Tanzania Bara;

(x) Programu ya Maboresho ya Mfumo wa Utumishi wa Umma yenye Mlengo wa Wananchi (*Citizen Centric Public Service Modernization Programme*) imeandaliwa kwa lengo la kuhakikisha huduma za Serikali zinakuwa bora, rahisi kufikiwa na zenye tija kwa wananchi. Programu hii itagharamiwa na fedha za ndani na imeombewa fedha za ugharamiaji kutoka Benki ya Dunia (IDA - 21);

(xi) Vikao vitatu (3) vya Kamati ya Rais ya Utekelezaji - PIC vimefanyika ambapo Miundo na Mgawanyo wa Majukumu kwa Wizara na Taasisi za Umma 33 imeidhinishwa kupitia Hati Idhini mpya iliyotolewa katika Tangazo la Serikali Na. 685 na 686 la tarehe 19 Desemba, 2025. Aidha, miundo na mgawanyo wa majukumu ya Taasisi za Umma 27 za nyongeza imechambuliwa na kujadiliwa katika vikao vya awali;

(xii) Tathmini ya mahitaji ya watumishi iliyofanyika kupitia mfumo wa e-Msawazo katika taasisi za umma 553 kati ya 571 kufikia Machi 2026, imebainisha kuwa kuna jumla ya watumishi 655,737 dhidi ya mahitaji halisi ya watumishi 930,423, hivyo kuwa na upungufu wa watumishi 274,686 kwa miaka mitano ijayo;

(xiii) Wadau na washiriki 1,670 kutoka kwenye Wizara 27, Idara Zinazojitegemea 27, Wakala za Serikali 27, Sekretarieti za Mikoa 26, Mamlaka za Serikali za Mitaa 184, Vyuo Vikuu 13 na Vyuo vya kati 28 wamewezeshwa katika matumizi ya Mfumo wa eMsawazo ili Wizara na Taasisi za Umma kuwa taarifa sahihi za mahitaji ya Watumishi;

(xiv) Wizara na Taasisi za Umma 356 kati ya 571 zimewezeshwa kuandaa na kuingiza taarifa za huduma wanazotoa katika Mfumo wa Daftari la Huduma za Serikali (GSD) ambapo huduma 529 zimeidhinishwa na kuanza kuonekana kwa watumiaji (wananchi) katika mfumo;

(xv) Uchambuzi wa nyaraka 30 za mifumo na viwango vya utendaji kazi Serikalini umefanyika, ikijumuisha Mikataba ya Huduma kwa Mteja, Mipango Mkakati, “Letter-heads” na nembo za Taasisi;

(xvi) Mwongozo wa Uandishi wa Nyaraka mbalimbali za Serikali umehuishwa ili kuboresha ubora na ufanisi wa mawasiliano Serikalini;

(xvii) Wizara na taasisi za umma 80 zimewezeshwa na kupatiwa elimu kuhusu masuala ya anuai za jamii ikiwemo UKIMWI, magonjwa yasiyoambukiza (MSY), jinsia na ulemavu;

(xviii) Huduma za ushauri wa kisheria zimetolewa kwa watumishi kutoka katika taasisi za umma 150 kuhusu masuala ya mashauri ya nidhamu na tafsiri ya Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 na Kanuni zake.

(xix) Mapitio ya Kanuni za utumishi wa Umma za mwaka 2022 yamefanyika;

(xx) Uhamasishaji wa maadili ya utendaji katika Utumishi wa Umma umefanyika kwa taasisi 42 ambapo jumla ya watumishi 23,370 walipatiwa mafunzo;

(xxi) Mipango ya Motisha na Mikataba ya Halibora za kazi ya taasisi na mashirika ya umma 23 imehuishwa na kuidhinishwa;

(xxii) Miundo ya maendeleo ya utumishi katika taasisi na mashirika ya umma 40 imehuishwa na kuidhinishwa. Aidha, miundo ya maendeleo ya utumishi ya kada chini ya Wizara 27 na Idara Zinazojitegemea nne (4) imehuishwa;

(xxiii) Semina Elekezi kwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri 56 imefanyika baada ya kuundwa kwa Serikali;

(xxiv) Taasisi za Umma 25 zimewezeshwa kuandaa na kutekeleza Mipango ya Rasilimaliwatu, Mipango ya Mafunzo na Mipango ya Urithishanaji Madaraka;

(xxv) Michakato ya Uendelezaji wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma ambayo ni Mipango ya Rasilimaliwatu; Urithishanaji Madaraka; na Uendelezaji Rasilimaliwatu imefanyiwa mapitio na kuboreshwa kwa ajili ya kutumika katika ujenzi wa mfumo wa kielektroniki wa Mipango ya Rasilimaliwatu (e-HRP);

(xxvi) Mfumo wa e-Watumishi umeboreshwa ili kuongeza ufanisi kwa watumiaji kwa kuwezesha waajiri kurekebisha malimbikizo yaliyoingizwa kimakosa na kuona malimbikizo yaliyopo Ofisi ya Rais-Utumishi, Wizara ya Fedha na yaliyolipwa;

(xxvii) Mfumo wa e-Watumishi umeboreshwa kwa kuongezwa kwa moduli ya Mipango ya Raslimaliwatu, Mafunzo kwa Watumishi wa Umma na Mipango ya Urithishanaji Ujuzi/Madaraka;

(xxviii) Mfumo wa e-Watumishi umeboreshwa ili kuwezesha waajiri kuongeza au kuhuisha taarifa za vituo vya kazi kwa watumishi na kuona nafasi wazi za uteuzi pamoja na watumishi wenye sifa za kuweza kujaza nafasi hizo;

(xxix) Mfumo wa Watumishi Portal umeboreshwa kwa kuwezesha waajiri kuongeza, kuhuisha au kuondoa masomo wanayofundisha walimu wa Shule za Msingi na Sekondari;

(xxx) Mazingira ya kuhifadhi Mifumo ya e-Watumishi, e-Utendaji na Watumishi Portal yamehuishwa kwa kufunga Seva 4 mpya;







1. Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Regina Qwaray akikabidhiwa ua na mtumishi wa Ofisi hiyo mara baada kuapishwa kuwa Naibu Waziri wa Ofisi hiyo iliyopo Mtumba Dodoma tarehe 18 Novemba, 2025.
2. Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI Bw. Juma Mkomi akimkabidhi cheti mmoja wa washiriki wa mafunzo ya Mfumo wa e-Watumishi yaliyojumuisha Maafisa Rasilimaliwatu na Maafisa Tawala kutoka Taasisi mbalimbali za Umma tarehe 1 Aprili, 2026 Jijini Dodoma.

(xxxi) Taasisi mpya 31 za kifedha zimeunganishwa katika Dirisha la Watumishi Portal (e-Mkopo) na kufanya idadi ya taasisi kufikia 64;

(xxxii) Mafunzo ya kujenga uwezo kuhusu matumizi, usimamizi na uendeshaji wa Mfumo wa e-Mrejesho yamefanyika kwa washiriki 456 katika Halmashauri 31, Hospitali za Wilaya 27 na Ofisi za Wakuu wa Wilaya 22 kwenye mikoa ya Kigoma, Katavi, Geita na Kagera. Aidha, kampeni za maadili katika taasisi 18 kutoka mikoa ya Kigoma na Kagera zimefanyika zikihusisha watumishi 26,032;

(xxxiii) Elimu ya maadili imetolewa kupitia vyombo vya habari ikiwemo Redio (E-FM) na Runinga (Televisheni cha AZAM (Morning Trumpet), TBC1 na ITV);

(xxxiv) Ufuatiliaji wa Uzingatiaji wa Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma umefanyika katika taasisi 32 kati ya 45 zilizopangwa. Aidha, ushauri wa kimaadili na utatuzi wa kero umefanyika katika Mikoa ya Kigoma na Kagera;

(xxxv) Ufuatiliaji na uchambuzi wa utekelezaji wa Mipango ya Utendaji Kazi na Mikataba ya Utendaji Kazi ya Taasisi iliyoandaliwa katika Mfumo wa e-Utendaji umefanyika katika taasisi za umma 256;

(xxxvi) Matangazo ya Magazeti ya Serikali 39 yaliwezeshwa kuchapishwa na Wakala ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali; na

(xxxvii) Kipindi maalum cha televisheni kiliandaliwa na kurushwa kwenye runinga kuhusu utekelezaji wa siku 100 za ahadi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.







1. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete akiwa ofisini mara baada ya kuapishwa kuwa Waziri wa Ofisi hiyo tarehe 18 Novemba, 2025 Mtumba Jijini Dodoma.
2. 1Naibu Waziri,Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Regina Qwaray akiwa na viongozi wa mbalimbali  wakati wakikagua maendeleo ya ujenzi wa mfereji wa umwagiliaji uliopo Meru kijiji cha Ngabobo wilaya ya Meru jijini Arusha.

## B. Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC)

**41. Mheshimiwa Spika;** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026 shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Watumishi wa umma 9,946 wamepatiwa mafunzo ya kuboresha utendaji kazi na utoaji huduma za serikali kwa wananchi. Kati ya watumishi hao 4,600 wamepatiwa mafunzo elekezi ya awali, 4,684 wamepatiwa mafunzo ya uongozi na maendeleo, menejimenti ya rasilimaliwatu na usimamizi wa Ofisi za umma, na watumishi 662 wamepatiwa mafunzo ya kujiandaa kufanya Mitihani ya Utumishi wa Umma;

(ii) Mafunzo ya muda mrefu yametolewa kwa wanachuo 10,661 katika fani za Utunzaji wa Kumbukumbu, Nyaraka na Taarifa, Uhazili, Menejimenti ya Rasilimaliwatu, Utawala wa Umma, na Usimamizi wa Manunuzi ya Umma;

(iii) Tafiti tumizi 14 zinaendelea, ushauri wa kitaalamu katika maeneo tisa (9) na machapisho 23 katika maeneo mbalimbali ya utumishi wa umma yametolewa kwa lengo la kuboresha utoaji huduma kwa wananchi na kuchangia katika utoaji wa maamuzi yanayozingatia matokeo ya utafiti;

(iv) Uratibu wa midahalo kwa njia ya mtandao katika eneo moja (1) kwa watumishi wa umma na wa Sekta Binafsi 494 umefanyika;

(v) Watumishi 41 wa Chuo wamewezeshwa kuendelea na mafunzo ya muda mrefu katika ngazi za Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu: Kati yao 9 wamewezeshwa shahada ya uzamivu, 25 shahada ya uzamili, na 7 shahada ya kwanza; na

(vi) Ujenzi wa jengo la ghorofa mbili (2) awamu ya kwanza katika Kampasi ya Tanga lenye vyumba vya madarasa 26, kumbi mbili (2) za mikutano, Ofisi za watumishi 24 na matundu ya vyoo 18 umekamilika kwa hatua ya boma.




1. Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, akiweka jiwe la msingi wa ujenzi wa Chuo cha Utumishi wa Umma Kampasi ya Tanga.







1. Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, akikagua jengo la Chuo cha Utumishi wa Umma Kampasi ya Tanga.
2. Mwonekano wa awali wa jengo la Chuo cha Utumishi wa Umma Kampasi ya Tanga.

## C. Watumishi Housing Investment (WHI)

**42. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 shughuli zilizotekelezwa na WHI ni pamoja na: -

(i) Ujenzi wa nyumba 54 za watumishi umekamilika, zikiwemo nyumba 15 za Sekta ya afya na 39 za Sekta ya Elimu katika wilaya zenye mazingira magumu. Kati ya hizo, nyumba 42 zimejengwa kwenye halmashauri za pembezoni na nyumba 12 zimejengwa jijini Dodoma;

(ii) Ujenzi wa nyumba 78 za Makazi kwa Watumishi wa Umma katika Wilaya zenye mazingira magumu kufikika umeanza, ambapo utekelezaji umefikia asilimia 30 na unatarajiwa kukamilika Julai, 2026;

(iii) Kuendelea na ujenzi wa nyumba 66 (badala ya nyumba 58 baada ya kufanya mapitio ya mchoro wa mradi) katika Mradi wa nyumba za ghorofa Kisasa Hilltop - Njedegwa Dodoma; Ujenzi umefikia asilimia 38 na unatarajiwa kukamilika Januari, 2027;

(iv) Kuendelea na ujenzi wa nyumba 101 katika Mradi wa ghorofa Mikocheni Dar es Salaam ambapo utekelezaji umefikia asilimia 70 na unatarajiwa kukamilika Julai, 2026;

(v) Thamani halisi ya Mfuko wa Faida imeongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 69.3 ikiwa ni ongezeko la asilimia 38 zaidi ya lengo la shilingi bilioni 50. Vilevile, idadi ya wawekezaji hai imeongezeka kwa asilimia 102, kutoka wanachama 7,553 mwezi Juni, 2025 hadi kufikia 15,276 mwezi Machi, 2026; na

(vi) Malipo ya viwanja 223 vya USA River jijini Arusha vilivyouzwa kwa mkopo hadi Machi, 2026 yamefikia shilingi bilioni 3.41 kutoka shilingi bilioni 2.29 Julai, 2025;







1. Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, akizungumza na wawekezaji wa Mfuko wa Uwekezaji wa Faida (Faida Fund) katika mkutano wa tatu wa Mfuko huo Januari 2026, Dar es Salaam.
2. Baadhi wa wawekezaji wa Mfuko wa Uwekezaji wa Faida (Faida Fund) wakifuatilia hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

## FUNGU 67 - OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

**43. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/26, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Fungu 67 ilitengewa jumla ya **shilingi 14,603,888,000.00**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 13,195,060,000.00** sawa na **asilimia 90.35** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 1,408,828,000.00** sawa na **asilimia 9.65** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**44. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2026 kiasi cha **shilingi 13,123,771,209.33** sawa na **asilimia 89.86** ya bajeti iliyoidhinishwa kilipokelewa. Kati ya fedha hizo, **shilingi 11,714,943,209.33** ni Matumizi ya Kawaida na **shilingi 1,408,828,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika kipindi hicho, kiasi cha **shilingi 12,425,831,209.33** sawa na **asilimia 94.68** ya fedha zilizopokelewa kilitumika, ambapo kiasi cha **shilingi 11,714,943,209.33** ni Matumizi ya Kawaida na **shilingi 710,888,000.00** kwa ajili Miradi ya Maendeleo.

**45. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hicho, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Jumla ya wasailiwa 91,126 wamepangiwa vituo vya kazi na ujazaji wa nafasi 12,722 unaendelea. Wasailiwa 41,102 wamehifadhiwa katika kanzidata, wakiwemo wanaume 21,899 na wanawake 19,203 wa kada mbalimbali baada ya kufaulu usaili wa mahojiano;

(ii) Maswali 77,863 ya kada 826 yamekusanywa, kuhakikiwa kutoka kwa wataalamu na kuhifadhiwa kwenye mfumo wa maswali (*Question Data Bank System)*;

(iii) Saili sita (6) za mchujo zimefanyika kufuatia waombaji kazi 845,042 kuwasilisha maombi ya kazi, kati ya hao waombaji 490,514 ni wanaume na 354,528 wanawake. Kati ya hao, Wasailiwa 9,836 walifanya usaili wa vitendo ambapo 6,928 ni Wanaume na 2,908 ni Wanawake;

(iv) Uhakiki wa vyeti 80,481 ulifanyika kwa kushirikiana na mamlaka husika (NECTA, RITA na TRA) ambapo vyeti 52 vilibainika kuwa vya kughushi na leseni 187 hazikukidhi vigezo vilivyowekwa;

(v) Ujenzi wa mfumo wa kupima haiba na tabia kwa wasailiwa (*Psychometric Test System*) umekamilika. Hatua inayoendelea ni ufanyikaji wa majaribio na hadi sasa jumla ya washiriki 62 wamefanyiwa majaribio ya mfumo wakiwemo watumishi waandamizi na viongozi 47 katika Utumishi wa Umma pamoja na wasailiwa 15 wa nafasi za uongozi;

(vi) Tathmini ya vituo vinavyotumika kwa usaili wa mchujo kwa njia ya kidijitali (*Online Aptitude Testing System - OATS*) imefanyika katika mikoa 31 kwa lengo la kuhakiki miundombinu ya vituo vilivyopo pamoja na kusanikisha (install) mfumo wa *OATS Desktop Application (ODA)*. Licha ya usaili wa kidigitali kufanyika katika ngazi ya mikoa, Sekretarieti ya Ajira imeanza kuendesha usaili katika ngazi ya Wilaya ambazo ni Muleba na Karagwe kwa Mkoa wa Kagera, Chato kwa Mkoa wa Geita, Bagamoyo kwa Mkoa wa Pwani, Kasulu kwa Mkoa wa Kigoma, Busega kwa Mkoa wa Simiyu na Bunda, Tarime na Butiama kwa Mkoa wa Mara;

(v) Maboresho ya mfumo wa Ajira Portal yamefanyika ili kuwezesha upangaji wa vituo vya kazi kwa wasailiwa waliofaulu usaili wa kada za Afya na Elimu katika ngazi ya vituo (Facility);

(vi) Mafunzo ya matumizi ya mfumo wa "Ajira Portal" yametolewa kwa washiriki 274 kutoka taasisi za umma 90 na kwa watumishi 101 wa Sekretarieti ya Ajira kuhusu matumizi, maboresho ya mfumo wa Ajira portal na mfumo wa kufanya usaili kwa njia ya mtandao (OATS);

(vii) Huduma za dawati la msaada na utatuzi kwa watumiaji wa mfumo wa 'Ajira Portal' zimetolewa ambapo jumla ya wadau 42,770 walihudumiwa. Kati ya hao, 19,802 walihudumiwa kwa njia ya simu, 22,968 walihudumiwa kwa njia ya barua pepe, na wadau 2,419 walihudumiwa katika ofisi za Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar;

(viii) Muundo mpya wa Sekretarieti umeidhinishwa, ambapo ofisi saba (7) za kanda zimeanzishwa pamoja na ofisi ya Zanzibar ili kusogeza huduma karibu na wananchi. Aidha, elimu kwa umma kuhusu mchakato wa ajira imetolewa kupitia vyombo vya habari, maonesho na taasisi za elimu ya juu.







1 - 2: Wasailiwa wa kada mbalimbali wakifanya usaili kwa vitendo kwenye maeneo mbalimbali ya vyuo husika walivyopangiwa.

## FUNGU 94 - OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA

**46. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/26, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma, Fungu 94 ilitengewa jumla ya **shilingi 9,677,775,000**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 9,177,599,000** sawa na **asilimia 94.83** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 500,176,000** sawa na **asilimia 5.17** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**47. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi, 2026 kiasi cha **shilingi 8,515,430,630.64** sawa na **asilimia 87.99** ya bajeti iliyoidhinishwa kilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo, **shilingi 8,015,254,630.64** ni Matumizi ya Kawaida na **shilingi 500,176,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**48. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma ilitekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Rufaa 154 kati ya rufaa 247 zilizopokelewa (sawa na asilimia 62.3) zimeamuliwa, rufaa 51 zinaendelea kuchambuliwa na rufaa 39 ziko katika hatua ya ufuatiliaji wa vielelezo kutoka Mamlaka husika;

(ii) Malalamiko 43 sawa na asilimia 48.9 ya malalamiko 88 yaliyopokelewa yameamuliwa na malalamiko 45 yapo katika hatua mbalimbali za uchambuzi. Wahusika walipewa fursa ya kusikilizwa kwa mujibu wa kanuni;

(iii) Warufani 40 na Warufaniwa sita (6) waliomba kufika mbele ya TUME walipatiwa fursa ya kusikilizwa kwa mujibu wa Kanuni ya 62(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022 ili kutoa ufafanuzi wa hoja zao;

(iv) Ukaguzi wa Uzingatiaji wa Sheria katika usimamizi wa Utumishi wa Umma kwa Taasisi 161 umekamilika. Kati ya taasisi hizo; Serikali Kuu 36, Mamlaka za Serikali za Mitaa 79, Taasisi za Umma 45 na taasisi moja (1) ilifanyiwa ukaguzi maalum;

(v) Elimu kwa wadau 1,213 kutoka Taasisi 15 kuhusu uzingatiaji wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya Utumishi wa Umma imetolewa kupitia mafunzo. Aidha, uhamasishaji umefanyika kupitia vipindi 25 vya televisheni, vipindi 26 vya redio, mitandao ya kijamii, magazeti nane (8) na tovuti ya Tume;

(vi) Watumishi wa umma 115 kutoka mamlaka za maji 85 wamejengewa uwezo kuhusu Mfumo wa Tume wa Uwasilishaji wa Taarifa za Kiutumishi na Ushughulikiaji wa Mashauri ya Nidhamu; na

(vii) Ujenzi wa jengo la Tume katika Mji wa Serikali Mtumba umefikia asilimia 93.





1. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete (meza kuu) akitazama moja ya nyaraka wakati Waziri huyo alipofanya ziara ya kikazi katika ofisi hiyo. Wengine ni Viongozi na Watendaji wa Ofisi ya Rais-UTUMISHI.
2. Kamati ya Tume ya Utumishi wa Umma ikiwa katika Mkutano wa Kupitia, Kujadili Rufaa na Malalamiko ya Watumishi wa Umma.

## FUNGU 04 - OFISI YA RAIS, IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA

**49. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/26, Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa ilitengewa jumla ya **shilingi 6,150,699,000.00**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 4,973,241,000.00** sawa na **asilimia 80.86** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 1,177,458,000.0**0 sawa na **asilimia 19.14** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**50. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **shilingi 4,309,650,041.14** sawa na **asilimia 70.07** zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo, **shilingi 3,251,666,836.50** ni Matumizi ya Kawaida na **shilingi 1,057,983,204.64** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**51. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Jumla ya majalada 778 yamerudufiwa na kuingizwa katika mfumo wa kidijitali yakijumuisha majalada 122 ya Ofisi ya Waziri Mkuu, 201 ya Ofisi ya Bunge, 198 ya iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na 257 ya kumbukumbu za utawala wa kikoloni wa Mjerumani;

(ii) Jumla ya taarifa rasmi za Bunge (Hansard) 2,011 zimekusanywa kutoka katika Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(iii) Mafunzo ya utunzaji bora wa kumbukumbu yametolewa katika Taasisi za Umma 15 kati ya 30 zilizopangwa kuwezeshwa;

(iv) Jumla ya kumbukumbu 297 za Waasisi wa Taifa letu (Mwl. Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume) zimetambuliwa, kukusanywa na kuhifadhiwa;

(v) Kumbukumbu 411 za Marais wastaafu zimetambuliwa, kukusanywa na kuhifadhiwa. Aidha, uchambuzi wa kumbukumbu za viongozi mbalimbali unaendelea ikijumuisha nyaraka zilizopokelewa kutoka Ubalozi wa Tanzania Addis Ababa, Ethiopia;

(vi) Jumla ya Kumbukumbu 4,000 zimehamishwa kutoka katika Taasisi za Umma 8 kati ya 10 kwenda Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu - Dodoma;

(vii) Mfumo wa Utunzaji Kumbukumbu za Kiutendaji (Keyword File Classification System) umewekwa katika Taasisi za Umma 40 kati ya 45 zilizopangwa. Aidha, Mfumo wa Masijala Mtandao (e-File Management System) umewekwa katika Taasisi 36 kati ya 45;

(viii) Taasisi za Umma 20 zimewezeshwa na kukamilisha Miongozo ya Kuhifadhi na Kuteketeza Kumbukumbu (Records Retention and Disposal Schedules - RRDS) kwa mujibu wa Sheria;

(ix) Watafiti 54 (37 wa ndani na 17 wa nje ya nchi) wamehudumiwa na kuwezeshwa kutumia nyaraka zinazostahili kwa ajili ya tafiti mbalimbali;

(x) Jumla ya nyaraka kongwe 71 za utawala wa kikoloni wa muingereza zikiwemo ramani, orodha za watumishi na majalada ya kiutendaji zimefanyiwa ukarabati (restoration);

(xi) Uwekaji Mfumo wa udhibiti wa uingiaji (Biometric Door Access Divices) katika Maghala ya kuhifadhia nyaraka Makao Makuu umekamilika. Aidha, uwekaji wa mfumo wa CCTV katika Kituo cha Kumbukumbu Kanda ya Ziwa-Mwanza unaendelea;

(xii) Mashine mbili (2) za kisasa (Heavy Duty scanners) kwa ajili ya urudufu wa nyaraka kidijitali zimenunuliwa;

(xiii) Jumla ya majalada 3,200 yamechambuliwa kwa ajili ya urudufu na kuingizwa katika mfumo wa Kuhifadhi Nyaraka Kidijitali, yakijumuisha majalada 1,200 ya iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na majalada 2,000 ya kumbukumbu za kiutawala wa kikoloni wa Uingereza; na

(xiv) Ujenzi wa jengo la Utawala Makao Makuu - Dodoma umefika asilimia 65.9.




1. Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria wakimsikiliza Afisa Kumbukumbu, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka, Bi. Maryam Ayoub (wa kwanza kushoto) alipokuwa akitoa maelezo kuhusu Vita vya Kagera kwa Wajumbe hao wakati wa ziara ya kikazi iliyolenga kukagua utekelezaji wa Mradi wa Kituo cha Kumbukumbu na Nyaraka Kanda ya Ziwa, Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela, Mwanza.

# MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2026/27 NA MASUALA MUHIMU YA KUZINGATIWA

**52. Mheshimiwa Spika,** Mpango na Bajeti kwa mwaka 2026/27 umeandaliwa kwa kuzingatia: Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050; Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025; malengo yaliyomo katika Mpango wa Nne wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2026/27 - 2030/31; Mpango wa Maendeleo Endelevu 2030 na Agenda Afrika 2063 na hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati akilihutubia Bunge la Kumi na tatu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 14 Novemba, 2025; Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2026/27. Shughuli zitakazotekelezwa na kila taasisi ni kama ifuatavyo:-

## OFISI YA RAIS - IKULU NA TAASISI ZAKE

### A. Ofisi ya Rais - Ikulu

**53. Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka 2026/27 Ofisi ya Rais, Ikulu imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Kutoa ushauri kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala ya Siasa, Uchumi, Jamii, Sheria, Diplomasia, Mawasiliano na Habari, Uhusiano wa Kikanda, Kimataifa na ushauri mwingine kwa lengo la kumsaidia Rais kufanya maamuzi;

(ii) Kuwezesha ratiba ya kila siku ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(iii) Kutoa huduma kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na familia yake;

(iv) Kuratibu, kuandaa na kushiriki mikutano 35 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, mikutano 20 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu na mikutano 15 ya Baraza la Mawaziri;

(v) Kuendesha vikao 10 vya mashauriano na wadau kwa ajili ya mapitio ya mfumo na uchambuzi wa sera mbalimbali na masuala ya kimkakati ya umma;

(vi) Kutoa mafunzo kuhusu utayarishaji na uwasilishaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri na uchambuzi wa sera kwa maafisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na waratibu wa shughuli za Baraza la Mawaziri;

(vii) Kuchambua na kutoa ushauri kwa Katibu Mkuu Kiongozi katika masuala ya kiuchumi, kijamii, kisheria, kiulinzi na kiusalama, kimataifa na masuala mengine yote yanayowasilishwa;

(viii) Kufanya mafunzo na ufuatiliaji wa Programu za Maboresho katika Sekta ya Umma nchini ikiwemo utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai katika ngazi za Wizara, Taasisi, Mikoa na Serikali za Mitaa;

(ix) Kupokea na kuchambua taarifa za robo mwaka na mwaka za utekelezaji wa Programu za Maboresho katika Sekta ya Umma nchini ikiwemo Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai;

(x) Kuendelea kujenga uwezo wa Taasisi za Umma kuhusu uzingatiaji wa utawala bora katika kutoa huduma kwa umma;

(xi) Kuratibu utekelezaji wa Mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai;

(xii) Kupokea, kupitia na kuchambua rufaa 240 na malalamiko 400 ya watumishi wa umma na wananchi;

(xiii) Kutoa mafunzo kwa viongozi 280 wa Serikali namna ya kushughulikia rufaa na malalamiko ya Watumishi wa Umma;

(xiv) Kuimarisha utekelezaji wa Uamuzi unaotolewa na Rais na Katibu Mkuu Kiongozi kwa Taasisi za Umma 60;

(xv) Kuimarisha uzingatiaji wa sheria na maelekezo yanayotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi na Mkuu wa Utumishi wa Umma yanayohusu masuala ya usimamizi wa utawala wa Utumishi kwenye Wizara, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

(xvi) Kuratibu na kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF na Programu ya Kujenga Uwezo wa Taasisi za Serikali Kupambana na Rushwa - BSAAT.

## B. Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)

**54. Mheshimiwa Spika;** katika Mwaka 2026/27, TAKUKURU imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Kufanya utafiti wa kitaifa wa hali ya utawala na rushwa nchini (*National Governance and Corruption Survey - NGACS*);

(ii) Kuimarisha matumizi ya fedha za umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha utekelezaji wake unazingatia thamani halisi ya fedha;

(iii) Kufanya uchunguzi wa majalada ya tuhuma za rushwa yanayoendelea pamoja na tuhuma mpya zitakazojitokeza;

(iv) Kuendesha Mashauri ya rushwa mahakamani kwa kibali cha mkurugenzi wa mashtaka;

(v) Kusakinisha data centre katika jengo jipya la Makao Makuu;

(vi) Kuendelea kutekeleza mpango wa TAKUKURU RAFIKI ili kuwashirikisha wadau wengi zaidi kwenye kuzuia na kupambana na rushwa;

(vii) Kutekeleza Mkakati wa Habari, Elimu na Mawasiliano (*Information, Education and Communication Strategy – IECS*) wa TAKUKURU ili kujenga uwezo na uelewa kuhusu rushwa, ufisadi na juhudi za Serikali katika kuzuia na kupambana na rushwa kwa makundi mbalimbali katika jamii kwa kutumia njia mbalimbali za uelimishaji na mawasiliano kuyashawishi makundi haya kuunga mkono na kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa nchini;

(viii) Kukamilisha na kuanza kutumia mfumo wa Takwimu na uchunguzi; na

(ix) Kufanya utafiti na uchambuzi wa mifumo ya kiutendaji na utoaji huduma katika ajira, elimu, afya na mifumo ya ukusanyaji mapato ya serikali ili kubaini maeneo yenye mianya ya rushwa na kushauri namna ya kuziba mianya hiyo.

## C. Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

**55. Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2026/27, TASAF imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Kukamilisha utambuzi na uandikishaji wa Kaya za Walengwa zinazokidhi vigezo ili kuingizwa kwenye Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Awamu ya Tatu katika Mamlaka za Utekelezaji 100 Tanzania Bara na Zanzibar;

(ii) Kuyajengea uwezo makundi mbalimbali kuhusu Mpango mpya yakiwemo ya viongozi na wawakilishi wa wananchi ili kuwa sehemu ya utekelezaji;

(iii) Kuhawilisha ruzuku kwa kaya za Walengwa 500,000 zinazokidhi vigezo katika Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Awamu ya Tatu katika Mamlaka za Utekelezaji 100 Tanzania Bara na Zanzibar;

(iv) Kufanya maandalizi ya utekelezaji wa Miradi ya Jamii ya Kutoa Ajira ya Muda kwa Kaya za walengwa yenye lengo la kuthibiti athari za Mazingira katika Mamlaka za Utekelezaji 10 zenye changamoto kubwa ya athari za kimazingira;

(v) Kuwezesha Jamii kutekeleza miradi ya kuendeleza miundombinu ya huduma za jamii katika sekta mbalimbali. Jumla ya miradi 723 itatekelezwa katika vijiji, mitaa na shehia katika Mamlaka za Utekelezaji 62 katika sekta za afya, elimu, maji, mazingira na ujasiriamali. Miradi hii itatekelezwa kupitia ufadhili wa Awamu ya Tano ya Mradi wa Kupunguza Umaskini Tanzania (Tanzania Poverty Reduction Project V – TPRP V) na mchango wa Serikali;

(vi) Kuimarisha miundombinu ya mifumo na kuunganisha mfumo wa walengwa na mifumo mingine ya Serikali ili kuweza kubadilishana taarifa kwa urahisi. Aidha, mfumo wa sasa utafanyiwa mapitio kwa ajili ya maboresho makubwa yanayoendana na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya taarifa za walengwa kwa Taasisi na wadau wangine; na

(vii) Kufanya Mapitio ya pamoja baina ya Serikali na Wadau wa Maendeleo kuhusu utekelezaji wa shughuli za Mpango na namna ya kuboresha maeneo mbalimbali yenye changamoto.

## D. Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)

**56. Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2026/276, Mamlaka ya Serikali Mtandao imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Kuendeleza usimamizi na kutathmini hali ya usalama wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwa taasisi 571, hatimaye kushauri maeneo ya kuboresha na kufuatilia utekelezaji wake ili kuhakikisha kuwa Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA Serikalini inafanya kazi na kutoa huduma kwa Taasisi za Umma na wananchi wakati wote kwa ufanisi na usalama;

(ii) Kuimarisha Mifumo ya TEHAMA jumuishi, Mifumo ya Kisekta na Mifumo ya Kitaasisi inayotumika ili iweze kuendelea kutoa huduma kwa ufanisi na usalama;

(iii) Kufanya uchambuzi, kusanifu na kujenga mifumo mipya ya kisekta kwa taasisi zenye taratibu za utendaji kazi zinazoendana kwa lengo la kupunguza wingi wa mifumo ya TEHAMA serikalini;

(iv) Kuunganisha Mifumo ya Taasisi za Serikali kwenye Mfumo wa kuwezesha Mifumo ya Serikali kuwasiliana na kubadilishana taarifa (Government Enterprise Service Bus - GovESB);

(v) Kufanya Utafiti na Ubunifu katika matumizi ya teknolojia mpya za TEHAMA ili kuibua huduma mpya kwa umma kupitia TEHAMA na kuwezesha matumizi sahihi na salama ya teknolojia mpya zinazoibuka;

(vi) Kuongeza wigo wa miundombinu ya Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (Government Network) ili kuifikisha katika Wilaya zote nchini na kuziwezesha Taasisi nyingi kutumia Mifumo inayopatikana kwenye Mtandao wa Serikali, ikiwemo mfumo wa Ofisi Mtandao (e-office), nk

(vii) Kuimarisha Mifumo ya Kimkakati, Kisekta na Kitaasisi ili kuhakikisha kuwa imetengenezwa na inatumika kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo iliyopo na kushauri maeneo ya kuboresha na kufuatilia utekelezaji wake;

(viii) Kusimamia, kuendesha na kuendeleza mifumo na miundombinu shirikishi ya TEHAMA serikalini, ikiwa ni pamoja na mtandao wa mawasiliano katika Mji wa Serikali Mtumba, vituo vya kuhifadhi mifumo na taarifa za Serikali, na vituo vya kujikinga na majanga;

(ix) Kuwajengea uwezo Watumishi katika kusimamia Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA katika Taasisi za Umma, pamoja na kutoa mafunzo kwa watumiaji kuhusu matumizi sahihi na salama ya Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA; na

(x) Kutoa ushauri wa kitaalamu na msaada wa kiufundi kwenye maeneo ya TEHAMA kwa taasisi za umma ili kuhakikisha viwango na miongozo inazingatiwa na kuwa na matumizi ya TEHAMA yenye tija na kupunguza gharama.

## E. Taasisi ya UONGOZI

**57. Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2026/27, Taasisi ya UONGOZI imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uzamili ya Uongozi kwa lengo la kuwajengea uwezo viongozi 40 katika maeneo ya maamuzi ya kimkakati, kusimamia rasilimaliwatu na rasilimali nyingine ili kuongeza tija;

(ii) Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uzamili ya Uongozi kwa lengo la kuwajengea uwezo viongozi 35 katika maeneo ya maamuzi ya kimkakati, kusimamia rasilimaliwatu na rasilimali nyingine ili kuongeza tija;

(iii) Kutoa mafunzo ya Cheti cha Uongozi kwa njia ya mtandao kwa lengo la kuwajengea uwezo viongozi 70 katika maeneo ya maamuzi ya kimkakati, matumizi ya takwimu, kusimamia rasilimaliwatu na rasilimali nyingine;

(iv) Kutekeleza programu maalum ya mafunzo ya Uongozi kwa lengo la kuwajengea uwezo viongozi wanaochipukia 35 katika maeneo ya maamuzi ya kimkakati, mawasiliano ya kimkakati, Uchambuzi wa Sera, na matumizi ya takwimu;

(v) Kutekeleza programu maalum ya mafunzo ya uongozi kwa wanawake viongozi waandamizi na viongozi wanaochipukia 100 kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kufanya maamuzi ya kimkakati, usimamizi wa rasilimali za Serikali na rasilimaliwatu. Vilevile, mafunzo haya yana lengo la kukuza vipaji vya uongozi kwa viongozi wanawake wanaochipukia;

(vi) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kupitia kozi 40 kwa lengo la kuwajengea uwezo viongozi 1,400 katika maeneo ya uongozi na maendeleo endelevu kwa ajili ya kuimarisha utendaji wao kwa kuzingatia mahitaji na maombi ya walengwa;

(vii) Kutekeleza programu maalum ya mafunzo ya uongozi kwa bodi 35 za Mashirika ya Umma, Taasisi za Umma na Wakala za Serikali kwa lengo la kuimarisha usimamizi na utendaji kwa Wakurugenzi wa Bodi 350. Mafunzo haya yatahusu uongozi wa kimkakati, usimamizi wa Mashirika ya Umma, usimamizi wa viashiria hatarishi, usimamizi wa rasilimali za umma na rasilimaliwatu;

(viii) Kufanya tafiti tumizi sita (6) kuhusu masuala ya uongozi na maendeleo endelevu ili kutoa ushauri wa kisera kwenye masuala muhimu yanayohusu maendeleo ya nchi ikiwemo maendeleo ya Nne ya Viwanda, Uchumi wa Buluu, na mabadiliko ya Tabianchi;

(ix) Kukamilisha uandishi wa kitabu kinachoelezea Wasifu wa maisha ya Hayati Rashid Mfaume Kawawa, aliyekuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kuendelea kuandika kitabu kinachoelezea Wasifu wa maisha ya Hayati Abeid Aman Karume, aliyekuwa Rais wa kwanza wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuweka kumbukumbu za viongozi mashuhuri wa Taifa letu katika maandishi;

(x) Kuandaa mikutano minne (4) ya kitaifa na miwili (2) ya kimataifa katika masuala ya uongozi kwa viongozi 550 kwa lengo la kubadilishana taarifa, maarifa na uzoefu na kuwaongezea uelewa wa masuala ya uongozi na maendeleo endelevu;

(xi) Kuandaa vipindi sita (6) vya runinga vitakavyoshirikisha viongozi waandamizi na wataalam mbalimbali wa ndani na nje ya nchi, juu ya uongozi na maendeleo endelevu;

(xii) Kutoa ushauri wa kitaalam kwa taasisi tano (5) za Serikali katika maeneo yanayohusu masuala ya uongozi na maendeleo endelevu; na

(xiii) Kutoa machapisho tisa (9) kuhusu masuala ya uongozi na maendeleo endelevu ikiwemo Tawasifu ya Hayati Rashidi Mfaume Kawawa.

## F. Wakala wa Ndege za Serikali

**58. Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2026/27, Wakala ya Ndege za Serikali imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa;

(ii) Kufanya matengenezo ya ndege zinazotoa huduma kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa;

(iii) Kulipia gharama za bima za ndege na za wanaanga;

(iv) Kugharamia uendeshaji wa Ofisi na kulipia gharama za vipuri na mafuta ya ndege; na

(v) Kutoa mafunzo ya kisheria kwa wanaanga kwa ajili ya kuhuisha leseni zao.

## G. Baraza la Kumshauri Rais Kuhusu Masuala ya Chakula na Kilimo

**59. Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2026/27 Baraza la Kumshauri Rais kuhusu Masuala ya Chakula na Kilimo (*Presidential Food and Agriculture Delivery Council-PFADC*), limepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kushauri kuhusu mikakati ya kuongeza ushiriki wa vijana katika kilimo;

(ii) Kushauri kuhusu Mikakati ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) katika mnyororo ya thamani ya mazao ya kipaumbele;

(iii) Kushauri kuhusu mikakati ya kuhamasisha uwekezaji wa mitaji katika sekta ya kilimo kutoka sekta Binafsi;

(iv) Kutoa ushauri kuhusu mbinu za kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha vijijini;

(v) Kushauri kuhusu Sera na Mikakati ya kuongeza ubunifu wa mifumo ya chakula; na

(vi) Kufanya mikutano ya wadau wa mazao ya kipaumbele (Ngano, Alizeti, Parachichi, Nyama na Maziwa).

**60. Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2026/27, Ofisi ya Rais, Ikulu: Fungu 20 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi 39,416,152,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri: Fungu 30 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi 1,382,937,948,000.00**. Kati ya fedha hizo **shilingi 1,256,299,943,000.00** sawa na **asilimia 90.84** ni Matumizi ya Kawaida na **shilingi 125,408,015,000.00** sawa na **asilimia 9.07** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa fedha za ndani na **shilingi 1,229,990,000.00** sawa na **asilimia 0.09** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa fedha za nje.

## FUNGU 33 - OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

**61. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2026/27, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inaendelea na vipaumbele vikuu viwili (2) ambavyo ni kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma kwa Taasisi na kwa wananchi ili kuweza kuwafikia kwa urahisi; na pili ni kuendelea kuwaelimisha viongozi wa umma kuhusu kuimarisha uwajibikaji wa pamoja miongoni mwa viongozi wa umma hususan katika ngazi ya halmashauri (wakuu wa idara na madiwani).

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2026/27, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kupokea na kuhakiki Matamko ya Rasilimali na Madeni kwa Viongozi wa Umma kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Sura 398;

(ii) Kuchunguza tuhuma za uvunjifu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Sura 398;

(iii) Kupokea malalamiko na taarifa za ukiukwaji wa maadili kwa mujibu wa sheria ya maadili ya viongozi wa umma kutoka kwa wananchi;

(iv) Kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Maadili ya Viongozi wa Umma;

(v) Kuelimisha viongozi wa umma na wananchi kwa ujumla kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Sura 398 na Hati ya Ahadi ya Uadilifu;

(vi) Kuanzisha na kuendeleza klabu za maadili katika shule na vyuo nchini; na

(vii) Kukamilisha ujenzi wa Ofisi Kanda ya Ziwa (Mwanza) na kuendelea na ujenzi wa Ofisi za Nyanda za Juu Kusini (Mbeya) na Mashariki (Morogoro) pamoja na kuanza kwa ujenzi wa Jengo la Kanda ya Kaskazini (Arusha).

**62. Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2026/27, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma katika mwaka 2026/27 inaomba kuidhinishiwa **shilingi 18,074,774,000.00** kwa ajili ya kutekeleza kazi zilizopangwa. Kati ya fedha hizo, **shilingi 15,074,774,000.0**0 sawa na **asilimia 83.40** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida, na **shilingi 3,000,000,000.00** sawa na **asilimia 16.60** kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

# FUNGU 32 - OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA NA TAASISI ZAKE

## A. Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

**63. Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka 2026/27, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kushughulikia vibali vya nafasi 45,000 za ajira mpya kwa ajili ya kujaza nafasi zitakazoidhinishwa katika Ikama za Taasisi za Umma;

(ii) Kuhakiki na kuidhinisha madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma katika taasisi 425;

(iii) Kufanya uhakiki wa watumishi na kusafisha taarifa zao za kiutumishi na mishahara (Staff Audit, Inspection and Data Cleaning) katika Taasisi 127 zinazotumia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (e-Watumishi);

(iv) Kuandaa na kufikisha kwa Waajiri Mwongozo wa Ikama na Bajeti ya Mshahara kwa mwaka 2027/28 kwa ajili ya utekelezaji;

(v) Kuhakiki na kuidhinisha mabadiliko ya taarifa za kiutumishi na mishahara katika Mfumo wa e-Watumishi kwa taasisi 524;

(vi) Kuidhinisha na kuunganisha Bajeti ya Mishahara ya taasisi 510 ya mwaka 2027/28 kabla ya kuwasilisha HAZINA na Bungeni;

(vii) Kutoa vibali vya ajira mbadala vya watumishi 7,124 wa kada mbalimbali;

(viii) Kuidhinisha maombi ya malimbikizo ya mishahara kwa wafanyakazi waliokoma utumishi kutoka kwa waajiri 200;

(ix) Kushughulikia malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi wa kudumu na kusimamia uchakataji wa orodha ya malipo ya mishahara kwa taasisi za umma 510;

(x) Kuwezesha taasisi 35 ambazo hazitumii Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (e-Watumishi) kuanza kutumia mfumo husika;

(xi) Kuanza utekelezaji wa Programu ya Maboresho ya Mfumo wa Utumishi wa Umma yenye Mlengo wa Wananchi. Programu hii itagharamiwa na fedha za ndani na nje kupitia Benki ya Dunia (IDA - 21);

(xii) Kuendesha vikao sita (6) vya Kamati ya Maboresho ya Taasisi za Umma (PIC);

(xiii) Kuhuisha Mfumo wa e-Watumishi kwa kuongeza huduma mtandao na kuhuisha teknolojia ya mfumo huo kufuatana na maoni ya wadau na mabadiliko ya teknolojia;

(xiv) Kuandaa Dashboard itakayotoa taarifa na ripoti mbalimbali kutoka Mifumo ya e-Watumishi, e-Msawazo, e-Utendaji na Watumishi Portal kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa takwimu sahihi katika ngazi mbalimbali za maamuzi katika Utumishi wa Umma;

(xv) Kuendeleza uunganishaji wa Mfumo wa e-Watumishi na mifumo mingine ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi pamoja na kusimamia usalama wa mfumo huo;

(xvi) Kuimarisha usimamizi, miundombinu, usalama, utoaji wa msaada wa kiufundi na matengenezo ya Mifumo ya e-Watumishi, e-Msawazo na Watumishi Portal;

(xvii) Kufanya uchambuzi wa utofauti wa mishahara katika Utumishi wa Umma na kuishauri Serikali kuhusu mkakati wa kuwianisha viwango vya mishahara kwa kipindi cha muda wa kati na muda mrefu;

(xviii) Kuratibu vikao vya Bodi ya Kima cha Chini cha Mshahara katika Utumishi wa Umma na Mabaraza ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma na Serikali Kuu;

(xix) Kuwezesha utekelezaji wa mipango ya motisha na miundo ya maendeleo ya utumishi na mishahara iliyoidhinishwa katika Taasisi na Mashirika ya Umma 70;

(xx) Kuwezesha usimamizi wa uzingatiaji wa maadili katika taasisi za umma kupitia njia mbalimbali pamoja na kampeni za kimaadili katika Sekretarieti za Mikoa miwili (2) na Halmashauri 30;

(xxi) Kutoa Mwongozo wa Mfumo wa Utekelezaji wa e-Msawazo;

(xxii) Kuwezesha uhamisho wa watumishi 7,000 na ujazaji wa nafasi 500 za uongozi kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi katika Utumishi wa Umma;

(xxiii) Kujenga uwezo wa usimamizi wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo kwa Mamlaka za Ajira 115 sambamba na matumizi ya mifumo ya kielektroniki ya utawala na usimamizi wa rasilimaliwatu;

(xxiv) Kushughulikia malalamiko 3,500 ya kiutumishi yanayotokana na ukiukwaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayosimamia Utumishi wa Umma;

(xxv) Kufanya mafunzo ya Mfumo wa Kielektroniki wa e-Mrejesho kwa taasisi za umma 16, kusakinisha Mfumo wa ‘’Shared Government Contact Center’’ katika taasisi za umma 20;

(xxvi) Kuandaa na kuboresha Miongozo ya Mifumo na Miundo (Mwongozo wa Uanzishaji wa Taasisi za Umma, Mwongozo wa Ushiriki wa Sekta ya Umma na Binafsi, Mwongozo wa Miundo ya Mgawanyo wa Majukumu katika Taasisi za Umma, Mwongozo wa Mfumo wa e - Msawazo, Mwongozo wa Nafasi na Samani za Ofisi katika Taasisi za Umma, Mwongozo wa Kuboresha Michakato ya Utoaji Huduma na Mwongozo wa Daftari la Huduma za Serikali);

(xxvii) iKuwezesha utekelezaji wa miundo ya mashirika ya taasisi 100 za umma;

(xxviii) Kufuatilia utekelezaji wa Viwango vya Usimamizi katika taasisi 100 za Umma;

(xxix) Kutoa taarifa ya kitaifa ya tathmini ya hali ya usimamizi wa utendaji kazi wa watumishi na taasisi za umma kwa kipindi cha mwaka 2025/26;

(xxx) Kufanya ufuatiliaji na kujenga uwezo wa utekelezaji wa Mfumo wa e-Utendaji katika Taasisi za Umma 571;

(xxxi) Kukamilisha mapitio ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma, Toleo la Tatu la mwaka 2009 na kutafsiri katika lugha ya Kiswahili;

(xxxii) Kukamilisha tathmini na kuanza kufanya mapitio ya Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma, 2008 kuendana na DIRA 2050 ;

(xxxiii) Kuratibu Mkutano wa Baraza Kuu la Wafanyakazi katika Utumishi wa Umma;

(xxxiv) Kuwezesha taasisi za umma katika utekelezaji na ujumuishwaji wa anuai za jamii mahali pa kazi katika Utumishi wa umma na kukamilisha Mwongozo wa Kudhibiti VVU, UKIMWI, Magonjwa Yasiyoambukiza na Changamoto za Afya ya Akili;

(xxxv) Kufanya mapitio ya Taratibu Bora za Uendeshaji wa Mashauri ya Nidhamu katika Utumishi wa Umma (Toleo la mwaka 2007);

(xxxvi) Kutoa huduma za kisheria katika masuala yanayohusiana na utawala na menejimenti ya rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma;

(xxxvii) Kuendeleza ujenzi wa Klabu ya Viongozi - Makao Makuu Dodoma eneo la Nzuguni awamu ya pili;

(xxxiii) Kuendeleza ujenzi wa nyumba ya kiongozi wa kitaifa mstaafu; na

(xxxix) Kutoa huduma kwa Viongozi wa Kitaifa Wastaafu 21 (Viongozi 10 na wajane 11) kwa mujibu wa sheria.

## B. Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC)

**64. Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2026/27, Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) kimepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuendeleza na kuboresha programu mpya 15 za mafunzo katika uongozi, usimamizi na utawala ili kuwajengea uwezo watumishi wa umma katika utendaji kazi na kutoa huduma bora kwa wananchi;

(ii) Kutoa mafunzo ya kujiandaa kufanya mitihani ya Utumishi wa Umma kwa watumishi 10,000 ili kuwajengea uwezo wa utendaji kazi na kutoa huduma bora kwa wananchi;

(iii) Kutoa mafunzo ya Uongozi na Maendeleo, Menejimenti na Usimamizi wa ofisi kwa watumishi wa umma 20,000 ili kuendeleza utumishi wa umma wenye sifa stahiki, uadilifu, uzalendo wa kitaifa, moyo wa kujituma, weledi, uwajibikaji, na kufanya kazi kwa bidii na kwa masilahi ya Taifa. Vilevile, mafunzo hayo yatatolewa kwa njia ya mtandao kwa watumishi wa umma 3,000;

(iv) Kutoa Mafunzo ya Awali katika Utumishi wa Umma wapya 10,000 ili kuwajengea uelewa wa kitendaji wa serikalini na misingi ya utumishi wa umma;

(v) Kuboresha miundombinu na mifumo ya ujifunzaji wa kidijitali ili kuongeza upatikanaji wa mafunzo kwa watumishi wa umma kwa gharama nafuu na kwa ufanisi;

(vi) Kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa washiriki 13,400 katika fani za Utunzaji wa Kumbukumbu, Uhazili, Kompyuta, Utunzaji wa Fedha za Umma, Menejimenti ya Rasilimaliwatu, Usimamizi na Manunuzi ya Umma, Uongozi na Utawala Bora;

(vii) Kutoa ushauri wa kitaalamu katika maeneo mbalimbali kwa Taasisi za Umma 12 kwa ajili ya kutambua changamoto halisi za utendaji na kuchangia katika utoaji wa maamuzi yanayozingatia matokeo ya tafiti;

(viii) Kufanya tafiti tumizi 14 na machapisho 20 katika maeneo ya Utumishi wa Umma yanayolenga kuboresha utoaji huduma kwa wananchi;

(ix) Kuratibu midahalo kwa njia ya mtandao katika maeneo matano (5) kwa watumishi wa umma na wa sekta binafsi;

(x) Kuwezesha mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 40 wa Chuo cha Utumishi wa Umma katika ngazi za Shahada ya Uzamivu, Shahada ya Uzamili na Shahada ya Kwanza;

(xi) Kukamilisha Ujenzi wa ya kampasi ya Tanga awamu ya kwanza unaojumuisha jengo la madarasa yenye uwezo wa kukalisha wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja; kumbi 2 za mikutano; na ofisi 24 za watumishi; na vyoo 18;

(xii) Ukarabati wa hosteli na nyumba za watumishi kwa kampasi ya Tabora ikiwa ni maandalizi ya kuhamishia huduma ya utoaji wa mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya Shahada ya Utunzaji wa Kumbukumbu na Uhazili; na

(xiii) Kuwezesha upatikanaji wa eneo kwa ajili ya ujenzi wa kampasi ya Mbeya.

## C. Watumishi Housing Investment (WHI)

**65. Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2026/27, Watumishi Housing Investment imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Kupitia Mradi wa Makazi kwa Watumishi wa Umma Wilayani Serikali itaendelea kukamilisha ujenzi wa nyumba 78, ambapo Nyumba 33 za watumishi wa Afya na nyumba 45 za watumishi Sekta ya Elimu;

(ii) Kuanza ujenzi wa nyumba 132 za Watumishi wa Umma Wilayani;

(iii) Kukamilisha ujenzi wa nyumba 66 na kuanza ujenzi wa nyumba 82 katika Mradi wa ghorofa Kisasa Hilltop, Njedegwa Dodoma;

(iv) Kukamilisha ujenzi wa nyumba 101 katika Mradi wa ghorofa Mikocheni Dar es Salaam;

(v) Kuanza ujenzi wa nyumba 280 katika Mradi wa ghorofa eneo la Jangwani Mbezi Beach - Dar es Salaam;

(vi) Kukuza Mfuko wa Faida hadi kufikia thamani halisi ya shilingi bilioni 100; na

(vii) Kutoa huduma za ujenzi na ushauri wa majenzi (*construction and consultancy services*) kwa taasisi za Serikali.

**66. Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2026/27, Fungu 32 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi 84,888,399,000.00**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 55,832,858,000.00** sawa na **asilimia 65.77** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 29,055,541,000.00** sawa na **asilimia 34.23** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

## FUNGU 67 - OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

**67. Mheshimiwa Spika;** katika mwaka wa fedha 2026/27 Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuwezesha kupatikana wataalam katika Utumishi wa Umma katika maeneo ya vipaumbele kama ifuatavyo:-

(i) Kufanya saili 22 kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuwapangia vituo wasailiwa waliofaulu;

(ii) Kusimamia saili 14 zilizokasimiwa kwa vyuo vikuu vya umma na saili 10 kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(iii) Kusimamia usaili wa kuandika kwa kada 600 na usaili wa vitendo kwa kada 250;

(iv) Kukusanya, kuchambua, kuhakiki na kuhifadhi maswali ya usaili 130,000 ya kada mbalimbali kwenye kanzidata ya maswali kutoka kwa wadau mbalimbali;

(v) Kuhuisha maswali 50,000 kutoka kwenye kanzidata ya maswali ambayo yamekwishatumika;

(vi) Kuwezesha uhakiki wa vyeti na nyaraka za msingi kubaini sifa za waombaji kazi;

(vii) Kuwezesha mafunzo elekezi kwa waajiri 100 kuhusu Mfumo wa Kupima Haiba na Tabia (*Psychometric Test System*) za wasailiwa pamoja na mafunzo kwa watumishi 146 wa Sekretarieti ya Ajira kuhusu mifumo mipya ya TEHAMA iliyojengwa;

(viii) Kuboresha na kusimamia Mfumo wa Kupima Haiba na Tabia (Psychometric Test System) na miundombinu ya TEHAMA katika vituo 40 vya usaili kwa njia ya mtandao (Online Aptitude Testing System - OATS);

(ix) Kuboresha mfumo wa Ajira Portal kwa kuunganisha na mifumo ya taasisi nyingine (Mabaraza ya Afya, TCU, mfumo wa walemavu chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na mfumo wa taarifa za wakimbizi);

(x) Kufanya kampeni tano (5) za kujenga uelewa kwa umma kuhusu mifumo ya TEHAMA ya Sekretarieti ya Ajira pamoja na kampeni 20 kuhusu michakato ya ajira; na

(xi) Kuanzisha ofisi za kanda saba (7) pamoja na kuwapatia watumishi vitendea kazi na mafunzo ili kuboresha utekelezaji wa majukumu.

**68. Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2026/27, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma (Fungu 67) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 19,292,567,000**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 17,883,739,000.00** sawa na **asilimia 92.70** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 1,408,828,000.00** sawa na **asilimia 7.30** ni kwa ajili ya mradi wa maendeleo.

## FUNGU 94 - OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA

**69. Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2026/27, Tume ya Utumishi wa Umma itatekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kufanya mikutano minne (4) ya Tume ya kisheria itakayojadili na kutolea uamuzi rufaa, malalamiko, taarifa za masuala ya Kiutumishi na masuala mengine ya kiutumishi kadri yatakavyopokelewa;

(ii) Kufanya Ukaguzi wa Kawaida katika Taasisi za Umma 300 na Ukaguzi Maalum katika Taasisi za Umma 10 kuangalia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma;

(iii) Kuelimisha Taasisi 574 katika Utumishi wa Umma kuhusu majukumu ya Tume na uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma;

(iv) Kuendeleza uboreshaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Kushughulikia Rufaa, Malalamiko, Ukaguzi wa Uzingatiaji wa Sheria na Uwasilishaji wa Taarifa za Kiutumishi (PSCMIS) kwa ajili ya kuongeza ufanisi kwenye utoaji wa haki;

(v) Kufuatilia na kuhakiki vielelezo vya rufaa na malalamiko kutoka kwa Warufani na Mamlaka za Nidhamu;

(vi) Kuimarisha ushirikiano kati ya Tume ya Utumishi wa Umma na Tume nyingine Barani Afrika na katika Ukanda wa SADC; na

(vii) Kuendeleza ushirikiano na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kutoa ufafanuzi na kujibu hoja za mashauri ya Warufani yanayofikishwa Mahakamani.

**70. Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2026/27, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma Fungu 94, inaomba kuidhinishiwa kiasi **shilingi 12,855,079,000.00** ili kutekeleza shughuli zilizotajwa hapo juu. Kati ya fedha hizo, **shilingi 12,354,903,000.00** sawa na **asilimia 96.11** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 500,176,000.00** sawa na **asilimia 3.89** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

## FUNGU 04 - OFISI YA RAIS, IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA

**71. Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2026/27 Ofisi ya Rais - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Kukusanya taarifa, kumbukumbu, nyaraka na machapisho mbalimbali yanayohusu historia ya nchi yetu kutoka katika Taasisi na watu binafsi;

(ii) Kutambua, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu, nyaraka na vitu vya Waasisi wa Taifa na Marais wengine wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(iii) Kuweka na kuhuisha mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu (Keyword filing system na e-file management system) katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma Serikalini;

(iv) Kuimarisha mifumo ya kielektroniki katika usimamizi wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu na nyaraka katika teknolojia ya kisasa kwa kuingiza nyaraka katika mfumo wa kidijitali (Digital Records Management and Preservation System) ili kurahisisha upatikanaji wake na kulinda nakala halisi;

(v) Kuwezesha taasisi za umma kuandaa miongozo ya kuhifadhi na kuteketeza kumbukumbu pamoja na kufanya tathmini (appraisal) ya kumbukumbu tuli za taasisi za umma zilizohifadhiwa katika Vituo vya Idara vya kuhifadhia kumbukumbu;

(vi) Kuzijengea uwezo taasisi za umma katika usimamizi wa kumbukumbu na nyaraka za Serikali kwa kuandaa mikutano kazi kwa menejimenti za taasisi za umma na mafunzo kazi kwa watumishi, waratibu na watunza kumbukumbu kuhusu sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya utunzaji wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka za Serikali;

(vii) Kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa utunzaji na uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka kwa maendeleo ya Taifa;

(viii) Kuweka na kuhuisha mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu katika Taasisi za Umma ili kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma Serikalini;

(ix) Kukagua, kuchambua na kuhamisha kumbukumbu tuli kutoka katika Taasisi za Umma na kuzihifadhi katika Vituo vya Kumbukumbu; na

(x) Kutoa ushauri wa kitaalam wa utunzaji wa kumbukumbu katika Taasisi za Umma.

**72. Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2026/27, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma Fungu 94, inaomba kuidhinishiwa kiasi **shilingi 12,855,079,000.00** ili kutekeleza shughuli zilizotajwa hapo juu. Kati ya fedha hizo, **shilingi 12,354,903,000.00** sawa na **asilimia 96.11** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 500,176,000.00** sawa na **asilimia 3.89** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

# MAJUMUISHO

**73. Mheshimiwa Spika,** katika kuhitimisha naomba nianze kwa salamu iliyoasisiwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayosema kwamba:

***KAZI NA UTU! TUNASONGA MBELE!!!***

**74. Mheshimiwa Spika,** maombi ya kuidhinishiwa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yanalenga kutafsiri kwa kina utayari na uongozi wa awamu ya sita, katika kuchapa kazi na kutambua kuwa maendeleo na mafanikio ya kweli hayawezi kufikiwa kama 'UTU' hautaliongoza Taifa hili kiutendaji. Hivyo ''Utumishi wa Umma unaowajibika, ulio jumuishi na wenye matokeo yanayoendana na matakwa ya wananchi'' ndio msingi wa kufikiwa maendeleo endelevu ya mama Tanzania. Hayo ni mojawapo ya maelekezo ya Ilani ya CCM kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025. Kuwa Serikali inatakiwa *"Kujenga Utumishi wa Umma wenye sifa stahiki, uadilifu, uzalendo wa kitaifa, moyo wa kujituma, weledi, uwajibikaji, na kufanya kazi kwa bidii na kwa masilahi ya Taifa."*

**75. Mheshimiwa Spika,** bajeti tunayoomba itasaidia Serikali kusimamia kwa ufanisi Utumishi wa Umma unganifu, wenye umahiri na ubunifu kupitia sera za utawala na usimamizi wa rasilimaliwatu, mifumo na miundo iliyoboreshwa ili kuchochea utoaji huduma wenye mlengo wa wananchi. Aidha, uidhinishaji huo utawezesha kuboresha mifumo, sera na taratibu za usimamizi wa rasilimaliwatu ili kuiwezesha Serikali kuendana na utekelezaji wa malengo ya DIRA 2050. Hatua hii itaimarisha usimamizi wa utekelezaji wa miradi ya kimkakati kwa ufanisi zaidi, sambamba na kuharakisha mageuzi ya kidijitali na ubunifu katika utoaji wa huduma za umma. Vilevile, maombi ya bajeti yatasaidia kukamilisha ujenzi wa majengo na mazingira wezeshi kwa watumishi walio katika mazingira magumu ambayo ni muhimu katika kuwawezesha kwa makazi bora na kulinda utu wa watumishi wa umma na haiba ya Serikali ili kuongeza ufanisi katika uratibu na utoaji wa huduma bora, jumuishi na endelevu kwa wananchi.

**76. Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa hati idhini, Ofisi ya Rais ikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaomba kuidhishiwa bajeti ili kutafsiri maono yake kuwa, Serikali yake itafanya kazi kwa kuzingatia dhana ya ***Kazi na Utu*** kama alivyosema alipokuwa anazindua Bunge la 13 **nanukuu:** *"...Namuomba Mwenyezi Mungu kuwa mwisho wa utumishi wa Awamu ya Sita usipimwe kwa vitu vitakavyoachwa, bali pia kwa tabasamu la utu litakaloachwa kwenye nyuso za Watanzania."* Ndio maana mipango iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako tukufu imejikita katika kuweka misingi ya utekelezaji wa mwelekeo huo.

**77. Mheshimiwa Spika,** Serikali inalenga kuacha tabasamu kwa watumishi wa umma ili huduma ziwe bora; itaendelea kuwajengea miundombinu bora ili wafurahie maisha na mazingira; kuongeza ajira kila mwaka ili kupunguza mzigo kwa wachache; kuwezesha mafunzo ili kupika wajuzi; kuboresha mfumo wa utoaji wa huduma katika utumishi wa umma ili ziwe na mlengo wa wananchi; TASAF mpango wake (PSSN III) umeidhinishwa na Bodi ya Benki ya Dunia, kwa hiyo bajeti 1. itakayoidhinishwa itaelekezwa kukamilisha kuanza kwa utekelezaji ili kutatua changamoto za kiuchumi na kijamii za kaya maskini nchini; haki za watumishi kupitia rufaa zinazopelekwa TUME zitashughulikiwa kwa msukumo zaidi ili kuleta tabasamu na kulinda UTU wa watumishi walioonewa kwa kufanyia kazi rufaa zao kwa ufanisi; na kumbukumbu, nyaraka na vitu vya waasisi wa Taifa zitawekwa katika hali ya kutoa elimu ya uzalendo kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

**78. Mheshimiwa Spika,** Utumishi wa Umma na Utawala Bora una mchango mkubwa katika maendeleo ya taifa, na ni dhahiri kuwa mchango endelevu wa watumishi wa umma utaliendeleza taifa na kuleta ustawi kwa Watanzania wote. Aidha, maendeleo haya yanatarajiwa kuongezeka kwa kuimarisha uchumi shindani na viwanda kwa manufaa ya watu, kama inavyosisitizwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP IV).

**79. Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii kumpongeza tena Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuliongoza taifa kwa kipindi cha pili cha awamu ya sita. Aidha tunapongeza jitihada zake katika kuimarisha utawala bora na kutuwezesha kuimarisha utumishi wa umma kuendana na wakati. Tunashukuru kwa maelekezo yake na uwezeshaji kifedha umesaidia hatua zaidi kupigwa kwenye kujenga uwezo na mifumo ya kimenejimenti na utoaji huduma ikiwemo matumizi sahihi na salama ya TEHAMA katika utoaji huduma serikalini.

**80. Mheshimiwa Spika,** maombi ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu pamoja na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, yanalenga kuviwezesha vyombo vya maamuzi, vya usalama, na mapambano dhidi ya rushwa nchini viweze kuchapa kazi zake. Rushwa haikubaliki na Serikali ya awamu ya sita inaichukia kwa vitendo. Hatutafumbia macho vitendo hivi. Hivyo, kupitishwa kwa bajeti hii ni mchango muhimu katika kuimarisha utendaji wa vyombo husika kwa manufaa ya Taifa. Aidha, Ofisi itahakikisha misingi ya utawala bora inaimarishwa katika ngazi zote, ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa viongozi wateule ili kujenga utumishi wa umma wenye weledi na unaozingatia uendelevu wa Serikali.

**81. Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Hati Idhini, nawajibika kuwasilisha mapitio ya utekelezaji mipango na bajeti ya Ofisi ya Rais Ikulu; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; na Ofisi ya Rais, Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa. Hivyo, nalihakikishia Bunge lako tukufu kuwa Mipango na Bajeti kwa Mafungu niliyoyataja yamezingatia vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Sita kwenye eneo la kuimarisha utendaji kazi katika Utumishi wa Umma na kuifanya nchi yetu iondokane na ukiukwaji wa maadili ya uongozi na kupunguza urasimu usio na lazima katika utoaji huduma kwa kufanya mapitio ya michakato ya utoaji huduma na hivyo kuongeza tija katika kutekeleza masuala yenye masilahi mapana kwa Taifa letu.

**82. Mheshimiwa Spika,** Baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2025/26 na Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora sasa naomba kuwasilisha rasmi mapendekezo ya maombi kwa mwaka 2026/27 kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | **Fungu 20: Ofisi ya Rais, Ikulu** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 39,416,152,000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **Sh.** | **39,416,152,000.00** |
| 2 | **Fungu 30: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 1,256,299,943,000.00 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 126,638,005,000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **Sh.** | **1,382,937,948,000.00** |
| 3 | **Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 15,074,774,000.00 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 3,000,000,000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **Sh.** | **18,074,774,000.00** |
| 4 | **Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 55,832,858,000.00 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 29,055,541,000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **Sh.** | **84,888,399,000.00** |
| 5 | **Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 17,883,739,000.00 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 1,408,828,000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **Sh.** | **19,292,567,000.00** |
| 6 | **Fungu 94: Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 12,354,903,000.00 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 500,176,000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **Sh.** | **12,855,079,000.00** |
| 7 | **Fungu 04: Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 5,731,623,000.00 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 2,397,458,000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **Sh.** | **8,129,081,000.00** |
| **MUHTASARI WA MAFUNGU YOTE** | | | |
| | Jumla ndogo kuu - Matumizi ya Kawaida | Sh. | 1,402,593,992,000.00 |
| | Jumla ndogo kuu - Miradi ya Maendeleo | Sh. | 163,000,008,000.00 |
| | **Jumla Kuu kwa Mafungu Yote** | **Sh.** | **1,565,594,000,000.00** |

**83. Mheshimiwa Spika na Wabunge wenzangu,** Jumla kuu ya Bajeti ninayoomba kwa Mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais (Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) kwa mwaka 2026/27 kama ilivyoanishwa katika jedwali hapo juu ni **shilingi 1,565,594,000,000.00**. Kati ya kiasi hicho **shilingi 1,402,593,992,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 163,000,008,000.00** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**84. Mheshimiwa Spika na Wabunge wenzangu;** mwisho naomba kuwasilisha maombi haya ili muweze kuyajadili na kuyaidhinisha.

**Asanteni kwa kunisikiliza, naomba kutoa hoja.**

**Ridhiwani J. Kikwete (Mb.)**

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS
(MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA)

# VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO 1: TAKWIMU ZA UCHUNGUZI NA MASHTAKA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2025 HADI MACHI, 2026

| MAELEZO | JUL. 2025 | AUG. 2025 | SEP. 2025 | OCT. 2025 | NOV. 2025 | DEC. 2025 | JAN. 2026 | FEB. 2026 | MAR. 2026 | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Malalamiko Yaliyopokelewa*** | 1,136 | 1,201 | 651 | 622 | 589 | 537 | 625 | 653 | 185 | **6,199** |
| Majalada yaliyokamilika | 74 | 27 | 61 | 40 | 56 | 64 | 58 | 55 | 144 | **579** |
| Majalada Yaliyopelekwa kwa NPS | 47 | 34 | 59 | 29 | 55 | 52 | 58 | 79 | 94 | **507** |
| Majalada yaliyorudi na kibali cha NPS | 43 | 12 | 16 | 22 | 18 | 33 | 24 | 18 | 38 | **224** |
| Majalada Yaliyofungwa | 39 | 75 | 21 | 30 | 22 | 33 | 8 | 24 | 32 | **284** |
| Kesi Mpya Zilizofikishwa Mahakamani | 61 | 37 | 19 | 31 | 22 | 9 | 30 | 33 | 63 | **305** |
| Kesi zilizoamuliwa Mahakamani: Kesi Zilizoshinda | 36 | 35 | 30 | 45 | 25 | 11 | 21 | 22 | 35 | **260** |
| Kesi zilizoamuliwa Mahakamani: Kesi Zilizoshindwa | 12 | 12 | 8 | 10 | 5 | 7 | 1 | 6 | 4 | **65** |
| Kesi zinazoendelea mahakamani | 386 | 358 | 316 | 337 | 247 | 251 | 279 | 315 | 339 | **339** |
| **Thamani ya Fedha Iliyookolewa (Tshs): Fedha Taslimu** | **155,569,635** | **241,075,521** | **59,979,282,726** | **1,794,245,974** | **22,510,712,875** | **88,170,803** | **24,813,643** | **122,850,468** | **236,766,944** | **85,153,488,589** |
| **Thamani ya Fedha Iliyookolewa (Tshs): Fedha zilizodhibitiwa** | **5,498,929,277** | **237,025,018** | **3,836,179,853** | **664,217,156** | **1,008,824,488** | **3,386,323,269** | **2,025,684,146** | **285,175,948** | **262,788,422** | **17,205,147,577** |
| **Thamani ya Fedha Iliyookolewa (Tshs): Jumla ya Fedha zilizookolewa** | **5,654,498,912** | **478,100,539** | **63,815,462,579** | **2,458,463,130** | **23,519,537,363** | **3,474,494,072** | **2,050,497,789** | **408,026,416** | **499,555,366** | **102,358,636,166** |

**NB: *** Siyo malalamiko yote yanayopokelewa yanahusiana moja kwa moja na rushwa.**

## KIAMBATISHO 2: ORODHA YA TAASISI ZA UMMA ZILIZOWEKEWA MFUMO WA MASIJALA MTANDAO (*KEYWORD FILE CLASSIFICATION SYSTEM*) KUANZIA JULAI 2025 HADI MACHI 2026

| NA. | JINA LA TAASISI |
|---|---|
| 1 | Halmashauri ya jiji la Dodoma |
| 2 | Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi. |
| 3 | Halmashauri ya Wilaya ya Geita |
| 4 | Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe |
| 5 | Halmashauri ya Wilaya ya Simiyu |
| 6 | Kituo cha Uwekezaji na Ukanda Maalumu wa Kiuchumi Tanzania (TISEZA) |
| 7 | Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) |
| 8 | Halmashauri ya Manispaa ya Tabora |
| 9 | Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe |
| 10 | Bodi ya Mazao Mchanganyiko |
| 11 | Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu |
| 12 | Ranchi ya NARCO |
| 13 | Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama |
| 14 | Wakala wa Nishati Vijijini (REA) |
| 15 | Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi |
| 16 | Halmashauri ya Wilaya ya Magu |
| 17 | Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga |
| 18 | Ofisi ya Rais, Wizara ya Maendeleo ya Vijana |
| 19 | Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Bunge (OCPD) |
| 20 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Igunga |

| NA. | JINA LA TAASISI |
|---|---|
| 21 | Wakala wa Misitu Tanzania |
| 22 | Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) |
| 23 | Halmashauri ya Wilaya ya Songwe |
| 24 | Halmashauri ya Mji Njombe |
| 25 | Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa |
| 26 | Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha |
| 27 | Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja |
| 28 | Chuo cha Diplomasia |
| 29 | Tume ya Nguvu za Atomic |
| 30 | Ofisi ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi katika Utumishi wa Umma |
| 31 | Halmashaur ya Wilaya ya Sikonge |
| 32 | Wakala wa Ndege za Serikali |
| 33 | Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga |
| 34 | Wakala wa Usafiri wa Ardhini Tanzania (LATRA) |
| 35 | Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma |
| 36 | Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi |
| 37 | Halmashauri ya Wilaya ya Mafia |
| 38 | Baraza la kumshauri Rai kuhusu Masuala ya Chakula |
| 39 | Halmashauri ya Wilaya ya Lindi |
| 40 | Wakala wa Misitu Tanzania |

## KIAMBATISHO 3: ORODHA YA TAASISI ZA UMMA ZILIZOWEKEWA MFUMO WA UTUNZAJI KUMBUKUMBU ZA KIUTENDAJI (*E – FILE MANAGEMENT SYSTEM*) KUANZIA JULAI 2025 HADI MACHI 2026

| NA. | JINA LA TAASISI |
|---|---|
| 1 | Halmashauri ya jiji la Dodoma |
| 2 | Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi. |
| 3 | Halmashauri ya Wilaya ya Geita |
| 4 | Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe |
| 5 | Halmashauri ya Wilaya ya Simiyu |
| 6 | Kituo cha Uwekezaji na Ukanda Maalumu wa Kiuchumi Tanzania (TISEZA) |
| 7 | Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) |
| 8 | Halmashauri ya Manispaa ya Tabora |
| 9 | Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe |
| 10 | Bodi ya Mazao Mchanganyiko |
| 11 | Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu |
| 12 | Ranchi ya NARCO |
| 13 | Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama |
| 14 | Wakala wa Nishati Vijijini (REA) |
| 15 | Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi |
| 16 | Halmashauri ya Wilaya ya Magu |
| 17 | Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga |
| 18 | Ofisi ya Rais, Wizara ya Maendeleo ya Vijana |

## KIAMBATISHO 4: ORODHA YA TAASISI ZILOZOWEZESHWA KUTENGENEZA MWONGOZO WA KUHIFADHI NA KUTEKETEZA KUMBUKUMBU KUANZIA JULAI 2025 HADI MACHI 2026

| NA. | JINA LA TAASISI |
|---|---|
| 1 | Tume ya Pamoja ya Fedha |
| 2 | Tume ya Mahakama |
| 3 | Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) |
| 4 | Shirika la Maendeleo ya Mafuta Tanzania (TPDC) |
| 5 | Mamalaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) |
| 6 | Chuo Kikuu cha Mzumbe |
| 7 | Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF) |
| 8 | Mfuko wa fidia kwa Wafanyakazi (WCF) |
| 9 | Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu – Mkwawa (MUCE) |
| 10 | Mamlaka ya Hifadhi ya Wanyamapori Tanzania (TANAPA) |
| 11 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali |
| 12 | Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) |
| 13 | Wakala wa Ununuzi Serikalini (GPSA) |
| 14 | Bodi ya Wakadiriaji gharama za Ujenzi na Wabunifu wajenzi (AQRB) |
| 15 | Wizara ya Ulinzi |
| 16 | Ofisi ya Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 17 | Wizara ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora |
| 18 | Taasisi ya Utafiti wa WanyamaporiTanzania |
| 19 | Bodi ya Usajili wa Makandarasi (ERB) |
| 20 | Wakala wa Ndege za Serikali |

## KIAMBATISHO 5: ORODHA YA TAASISI ZA UMMA ZILIZOFANYIWA MAFUNZO YA UTUNZAJI WA KUMBUKUMBU KUANZIA JULAI 2025 HADI MACHI 2026

| NA. | JINA LA TAASISI |
|---|---|
| 1 | Chuo cha Utumishi wa Umma - Zanzibar |
| 2 | Wizara ya Fedha |
| 3 | Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) |
| 4 | Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF) |
| 5 | Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) |
| 6 | Chuo cha Maendeleo ya Mipango Vijijini (IRDP) |
| 7 | Mamlaka ya dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA) |
| 8 | Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC) |
| 9 | Jeshi la Polisi Tanzania |
| 10 | Wizara ya Habari,Utamaduni,Sanaa na Michezo |
| 11 | Ubalozi wa Afrika Mashariki |
| 12 | Bodi ya Usajili wa Makandarasi (ERB) |
| 13 | Wizara ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora |
| 14 | Wakala wa Ununuzi Serikalini (GPSA) |
| 15 | Shirika la Mzinga |




**Jengo la Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**